KUCHUNGUZA USAWIRI WA MWANAMKE KATIKA RIWAYA: MFANO WA RIWAYA YA UTENGANO

STANLEY JULIUS SARO

TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2017

UTHIBITISHO

Aliyetia saini yake hapa chini, anathibitisha kuwa, amesoma tasnifu hii iitwayo "***Kuchunguza Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya: Mfano wa Riwaya ya Utengano***" na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sehemu ya masharti ya kutunukiwa Digrii ya Uzamili (M.A) Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

…….

Dkt. Mohammed Omary Maguo

(Msimamizi)

……..

Tarehe

HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote sehemu yoyote ile ya tasinifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

TAMKO

Mimi, **Stanley Julius Saro** nathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au nyingine yoyote.

……

Sahihi

……

Tarehe

TABARUKU

Napenda kuitabaruku tasinifu hii kwa mke wangu kipenzi bi. Elika Kiangi.

SHUKURANI

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya na salama katika kipindi change chote cha masomo. Kwa hakika Mwenyezi Mungu anastahili kushukuriwa sana kwani yeye ndiye muweza wa kila jambo na humpandisha amtakaye na pia humshusha amtakaye. Mimi kwa upande wangu ninaona kuwa Mwenyezi Mungu amenipandisha katika daraja la juu katika elimu na ninamuomba aendelee kunipa afya na salama ili niendelee kusoma katika ngazi za juu zaidi.

Pia, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa msimamizi wangu Dkt. Mohamed Omary Maguo kwa kuisimamia kazi hii tangu mwanzo mpaka mwisho. Daktari hakuchoka katika kunielekeza mara nyingi kadri ilivyowezekana mpaka nikaweza kufikia hatua ya kuhitimu masomo ya shahada ya Uzamili.

Kipekee napenda pia nimshukuru mke wangu Elika Kiangi kwa uvumilivu wake mkubwa kutokana na muda mwingi kuwa katika masomo na hivyo kutoonana na siku kadhaa. Uvumilivu wake ndio ulionipa ujasiri wa kusoma kwa juhudi na maarifa mpaka leo hii ninakamilisha masomo yangu. Pia, ninawashukuru sana watoto wangu Julius Stanley, Verynice Stanles, Whitness Stanley na Fabian Stanley kwa kuvumilia kukosekana kwangu nyumbani nikiwa katika masomo.

IKISIRI

Mada ya utafiti huu ni kuchunguza usawiri wa mwanamke katika riwaya kwa kurejelea riwaya ya *Utengano*. Mada hii imefungamana vizuri na lengo kuu la utafiti huu lililovunjwa katika malengo mahususi mawili. Malengo hayo ni kuchambua usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Utengano* na kubainisha uhalisia wa usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Utengano* kwa jamii ya leo. Ili kutimiza malengo haya mahususi ya utafiti wetu tulikusanya data kwa kutumia mbinu za usomaji makini na upitiaji wa nyaraka maktabani na kuzichambua kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na nadharia ya Ufeministi.

Utafiti umebaini kuwa mwanamke anasawiriwa katika hali mbalimbali ndani ya riwaya teule ikiwa ni pamoja na mwanamke ni kiumbe tegemezi, mwanamke ni kiumbe mpenda starehe, mwanamke ni malaya, mwanamke ni kiumbe muovu na mwanamke ni kiumbe jasiri. Pia imebainika kuwa mwanamke anasawiriwa kama kiumbe mchapakazi, kiumbe wa ndani, kiumbe mtiifu na kiumbe wa kuteswa. Usawiri huu wa mwanamke katika riwaya ya Utengano unaonekana kuwa na uhalisia katika maisha ya leo ya jamii kwani bado mwanamke anaguswa na usawiri huu katika maisha yake ya kila siku.

YALIYOMO

UTHIBITISHO ..... **ii**

HAKIMILIKI ..... **iii**

TAMKO ..... **iv**

TABARUKU ..... **v**

SHUKURANI vi

IKISIRI ..... **vii**

YALIYOMO ..... **viii**

SURA YA KWANZA 1

1.0 UTANGULIZI 1

1.1 Utangulizi 1

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti 1

1.3 Tatizo la Utafiti 3

1.4 Lengo Kuu la Utafiti 4

1.4.1 Madhumuni Mahususi 4

1.4.2 Maswali ya Utafiti 4

1.5 Umuhimu wa Utafiti 5

1.6 Mipaka ya Utafiti 6

1.7 Mpangilio wa Tasinifu 6

SURA YA PILI **8**

2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA **8**

2.1 Utangulizi 8

2.2 Usawiri wa Mwanamke katika Kazi za Fasihi kwa Ujumla 8

2.3 Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya za Kiswahili 16

2.4 Mkabala Wa Kinadharia 21

2.4.1 Utangulizi 21

2.4.2 Nadharia ya Ufeministi 21

2.5 Hitimisho 26

SURA YA TATU 27

3.1 MBINU ZA UTAFITI 27

3.1 Utangulizi 27

3.2 Eneo la Utafiti 27

3.3 Usanifu wa Utafiti 27

3.4 Aina ya Data Zilizokusanywa 28

3.1.1 Data za Msingi 28

3.1.2 Data za Upili 28

3.2 Mbinu za Ukusanyaji wa Data 29

3.2.1 Usomaji Makini 29

3.2.2 Upitiaji wa Nyaraka 29

3.3 Sampuli na Usampulishaji 30

3.4 Uchambuzi wa Data 30

3.5 Hitimisho 31

SURA YA NNE 32

3.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI 32

4.1 Utangulizi 32

4.2 Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya Utengano 32

4.2.1 Mwanamke Kiumbe Tegemezi 33
4.2.2 Mwanamke ni Mpenda Starehe 34
4.2.3 Mwanamke ni Malaya 36
4.2.4 Mwanamke ni Kiumbe Muovu 38
4.2.5 Mwanamke ni Kiumbe Jasiri 41
4.2.6 Mwanamke ni Kiumbe Mchapakazi 43
4.2.7 Mwanamke ni Kiumbe wa Ndani 45
4.2.8 Mwanamke ni kiumbe Mtiifu 47
4.2.9 Mwanamke ni Kiumbe wa Kuteswa 49
4.3 Hitimisho 51
SURA YA TANO 53
5.0 HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO 53
5.1 Utangulizi 53
5.2 Muhtasari 53
5.2.1 Usawiri wa Mwanamke katika Utengano na Uhalisia Wake kwa Jamii 53
5.3 Hitimisho 55
5.4 Mapendekezo 56
MAREJELEO 57

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Utangulizi

Utafiti huu unachunguza Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya *Utengano* iliyoandikwa mwaka 1980 na mwandishi Said Ahmed Mohamed. Said Ahmed Mohamed ni Profesa wa taaluma za fasihi ambaye amechapisha vitabu vya riwaya, tamthiliya, mashairi na hadithi fupi kwa kiwango kikubwa kabisa. Riwaya hii inahusu utengano uliotokea katika familia ya Bwana Makusuudi kutokana na hila zake mwenyewe na watu wa nje kama Farashuu na Binti Kocho. Kupitia utengano huo tumeweza kubainisha namna mwanamke anavyosawiriwa katika riwaya hii na kuelezea uhalisia wake kwa jamii ya leo.

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Ngaiza (2003; 2004) anaeleza kwamba, harakati za kumkomboa mwanamke kutoka katika makucha ya mfumo dume zinashindwa kwenda kwa kasi inayostashiki kwa sababu mfumo dume umeota mizizi kiasi cha kupenya mpaka katika utamaduni na kuwa sehemu muhimu ya utamaduni huo. Matteru (1982) anasema kwamba, kutokana na hali hii mwanamke bado ameendelea kusawiriwa kama mtu kahaba, mzinzi, asiye mwaminifu, mdanganyifu na muovu katika kazi mbalimbali za fasihi hususani riwaya ya Kiswahili. Anaendelea kueleza kwamba, kwa upande mwingine zipo kazi zinazomsawiri mwanamke kama kiumbe mchapakazi, mlezi wa familia, mkulima hodari, mbunifu wa maendeleo, mshauri kwa familia, jamii na kadhalika. Hata hivyo, tunapotazama usawiri huu wa mwanamke ambao unaonekana kuwa ni

chanya bado tunauona kuwa unamtazama mwanamke kama kiumbe anayestahili kuwa ndani kwamba yeye ni mama wa nyumbani na mwanaume ndiye mtu wa umma yaani mahali pake ni nje katika shughuli mbalimbali za maendeleo na ujenzi wa taifa (Ngaiza, 2004; Shao, 2003; 2004; 2010).

Lyatuu (2011) alifanya utafiti linganishi juu ya namna waandishi wanaume na wanawake wanavyomsawiri mwanamke katika kazi zao. Utafiti wake unaonesha kwamba, waandishi wanawake wamepiga hatua kubwa katika kumsawiri mwanamke katika hali chanya ikilinganishwa na watunzi wanaume ambao wengi wao humsawiri mwanamke katika hali hasi kwa kiwaango kikubwa. Hata hivyo, matokeo ya utafiti wake yanakiri kwamba wapo baadhi ya waandishi wanawake ambao wanamsawiri mwanamke katika hali ya uhasi kuwa mwanamke ni kiumbe muovu na dhaifu mbele ya mwanamume. Hii inatokana na hali halisi ya mfumo dume ambao ndio uliotawala katika maisha ya kila siku ya jamii nyingi za Afrika ile ya Tanzania ikiwapo (Mwaipopo, 1990). Kazi ya fasihi ni zao la jamii na daima husawiri kile ambacho kinatokea katika maisha ya kila siku ya jamii. Hivyo, hata kama baadhi ya watunzi wanawake wa kazi za fasihi watajitahidi kumsawiri mwanamke kinyume na uhalisia uliopo katika jamii ni dhahiri kwamba jitihada zao zitajikuta zinamsawiri mwanamke katika hali ya uduni.

Katika kipindi cha utandawazi, serikali mbalimbali duniani hasa zile za mataifa yanayoendelea zimepewa masharti na mataifa yanayoendelea pamoja na Benki ya Dunia na Mfuko wa Fedha wa Kimataifa kuhakikisha kwamba wanawake wanapewa nafasi sawa na wanaume katika sekta zote kama sehemu ya kutimiza vigezo vya

kupata misaada (Shao, 2004). Serikali za nchi hizi zimefanya kazi hiyo ya kutekeleza masharti ya mashirika hayo na kuandaa mipango ambayo inawezesha wanawake kupata nafasi sawa na wanaume katika sekta za uongozi, elimu, kupata huduma za afya, kumiliki mali na ajira. Kwa mfano, katika nchi ya Tanzania serikali ilianzisha utaratibu wa kuwa na viti maalumu katika bunge kwa ajili ya wanawake ili waweze kushiriki katika vikao vya bunge kama waheshimiwa wabunge. Viti hivi vimetoa fursa kwa wanawake kuonesha uwezo wao kwamba nao wanaweza kufanya ama kushiriki katika uongozi kama ilivyo kwa wanaume pale tu watakapowezeshwa na kupatiwa fursa za kufanya hivyo (Shao, 2004).

Kazi za fasihi haziko nyuma katika kusawiri mambo mbalimbali yanayotokea katika jamii. Suala hili la wanawake nao kushiriki katika nafasi mbalimbali za uongozi nalo limesawiriwa katika kazi za riwaya hasa zile za kitandawazi. Baada ya kuligundua hili tukaamua kufanya utafiti wa kina ili kuweza kuona taswira ya mwanamke katika riwaya ya *Utengano*.

1.3 Tatizo la Utafiti

Usawiri wa taswira ya mwanamke katika kazi za fasihi umejitokeza tangu pale tu mwanadamu alipoumbwa na kuanza kuandaa na kushiriki katika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali. Pamoja na mambo mengine mwanamke amesawiriwa katika hali ya uhasi kwa kipindi kirefu katika kazi hizo bila ya kuthamini mchango chanya wa mwanamke katika maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla. Hata hivyo, katika miaka ya hivi karibuni kumekuja wimbi kali la uhamasishaji na ukombozi wa mwanamke katika kuhakikisha kwamba anapata haki sawa na mwanamme. Katika

kuchunguza kama azma hii adhimu imefanikiwa watafiti kadhaa wamehakiki kazi za fasihi na kueleza taswira ya mwanamke kwa ujumla. Miongoni mwao ni Mulokozi (1982), Matteru (1982), Lyatuu (2011), Kamba (2012) na Ramadhani (2013). Kati ya watafiti wote hawa hakuna hata mmoja ambaye amechunguza taswira ya mwanamke katika riwaya ya *Utengano* ili kuona namna mwanamke alivyosawiriwa katika riwaya hiyo. Utafiti huu umechunguza taswira ya mwanamke katika riwaya ya *Utengano* iliyoandikwa mwaka 1980 wakati mapambano ya harakati za kudai haki sawa kati ya wanawake na wanaume yamepamba moto katika nchi za Afrika na duniani kote kwa jumla.

1.4 Lengo Kuu la Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza taswira ya mwanamke katika riwaya ya *Utengano* ya mwandishi Said Ahmed Mohamed.

1.4.1 Madhumuni Mahususi

Utafiti huu una jumla ya madhumuni mahususi mawili ambayo ni haya yafuatayo:

i) Kuchambua usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Utengano*.

ii) Kubainisha uhalisia wa taswira ya mwanamke katika riwaya ya *Utengano* kwa jamii ya leo.

1.4.2 Maswali ya Utafiti

Maswali ya utafiti ni sehemu muhimu katika kusaidia madhumuni mahususi kutimiza kazi yake iliyokusudiwa na kama ilivyokusudiwa. Yafuatayo ni maswali ya utafiti wetu.

i) Mwanamke anasawiriwa vipi katika riwaya ya Utengano?

ii) Usawiri wa mwanamke katika riwaya ya Utengano una uhalisia gani kwa jamii ya leo?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Huu ni utafiti wa kitaaluma ambao bila ya shaka yoyote ile unakusudiwa kutoa mchango muhimu katika maendeleo ya taaluma ya fasihi ya Kiswahili na nje ya taaluma hii pia. Katika upande wa taaluma utafiti huu utamika kama rejeleo muhimu katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili hususani riwaya. Watakaorejelea kazi hii ni wanafunzi wanaosoma katika ngazi ya shahada ya kwanza, uzamili na uzamivu. Vile vile, wahadhiri nao watarejelea utafiti huu katika harakati zao za kuandika makala, vitabu na katika mijadala yao mbalimbali ya kitaaluma.

Kwa upande wa nadharia, utafiti huu utakuwa ni sehemu muhimu ya kuthibitisha kwamba nadharia za uhakiki wa kifasihi ni muhimu sana katika kukamilisha kazi yoyote ile ya utafiti wa kitaaluma. Miongoni mwa nadharia itakayothibitishwa ni ile ya Ufeministi ambayo inatoa msisitizo kwamba wanadamu wote ni sawa na hakuna aliye bora kuliko mwingine awe mwanamke au mwanaume. Hivyo, nadharia hii inataka kuona kwamba mwanaume na mwanamke wote wanapewa haki sawa katika maisha yao ya kila siku. Kupitia utafiti huu nadharia hii itathibitishwa vilivyo pamoja na mapungufu iliyonayo pia yatawekwa bayana.

Kwa upande wa siasa, utafiti huu utakuwa rejeleo muhimu kwa watunga sera hasa zile zinazohusiana na na masuala ya jinsia katika kutathimini mafanikio na hima

mbalimbali katika maendeleo ya nafasi ya mwanamke katika jamii. Hii itawasaidia kuwa wabunifu zaidi katika kuandaa mikakati na sera madhubuti zitakazoleta tija na ufanisi katika harakati za kuimarisha usawa miongoni mwa wanajamii.

Kwa upande wa utamaduni, utafiti huu utakuwa na dhima ya kuonesha namna utamaduni wa jamii unavyobadilika taratibu kwa kukubali mabadiliko ambayo yanatokea katika karne hii ya ishirini na moja ijulikanayo kama karne ya Sayansi na Teknolojia. Mwaipopo (1990) anaeleza kwamba utamaduni wa jamii si kitu kinachoweza kubadilika mara moja kama ilivyo kwa mambo mengine bali hubadilika taratibu. Kwa mantiki hii utafiti huu utakuwa rejeleo muhimu kwa wanaojifunza na kutafiti masuala yanayohusiana na utamaduni wa jamii ya Watanzania na jamii nyinginezo duniani.

1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu unalenga kuchunguza taswira ya mwanamke katika riwaya ya *Utengano* tu. Hivyo basi, utafiti huu hautashughulikia masuala ya wanawake katika muktadha wa taaluma nyingine kwa ujumla wake bali katika muktadha wa kifasihi tu. Hii itatusaidia kupata picha kamili ya taswira ya mwanamke katika riwaya teule.

1.7 Mpangilio wa Tasinifu

Tasinifu itakayoaandikwa itakuwa na jumla ya sura sita ambapo sura ya kwanza imeeleza juu ya utangulizi wa jumla wa utafiti. Katika sura hii kumeelezwa vipengele vya usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, lengo kuu la utafiti, madhumuni mahususi ya utafiti na maswali ya utafiti. Pia, vipengele vya umuhimu

wa utafiti, mipaka ya utafiti, vikwazo na utatuzi wa vikwazo nao umeelezwa katika sura hii. Sura ya pili inahusu utalii wa kazi tangulizi kuhusiana na mada ya utafiti. Sura ya tatu imewasilisha nadharia za uhakiki wa fasihi. Sura ya nne imewasilisha mbinu za utafiti. Sura ya tano imewasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti. Sura ya sita imetoa hitimishi, muhtasari na mapendekezo ya utafiti.

SURA YA PILI

2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

2.1 Utangulizi

Katika utafiti huu tumepitia kazi tangulizi katika tanzu mbalimbali za fasihi ambazo zinazungumzia juu ya usawiri wa mwanamke ili kuweza kubainisha pengo la kiutafiti ambalo ndilo haswa tulilolitafiti. Tumeanza na kazi tangulizi zilizochunguza usawiri wa mwanamke katika fasihi kwa ujumla halafu kazi tangulizi katika riwaya za Kiswahili.

2.2 Usawiri wa Mwanamke katika Kazi za Fasihi kwa Ujumla

Utafiti na uhakiki kuhusu taswira ya mwanamke katika kazi za fasihi umefanywa na wanataalimu kadhaa kwa nia na makusudio tofautitofauti. Kwa kuwa utafiti huu unahusu taswira ya mwanamke katika riwaya ni vema tupitie machapisho kumhusu mwanamke katika tanzu mbalimbali za fasihi ya Kiswahili kisha tumalizie na riwaya. Hii itatusaidia kupata picha ya jumla juu ya usawiri wa mwanamke katika fasihi na kisha kutuwezesha kupata maarifa ya kuupeleka mbele utafiti huu.

Matteru (1982) anaeleza kwamba taswira ya mwanamke inayojitokeza katika vipera vingi vya fasihi simulizi ni ile inayomuonesha kuwa ni mama wa nyumbani, chombo cha starehe, asiyezaa na hana heshima yoyote katika jamii. Tunakubaliana na mawazo ya Materu (ametajwa) kuwa katika fasihi simulizi mwanamke anaswiriwa katika hali ya uduni na kwamba ni chombo cha starehe kwa mwanaume. Hata hivyo, si kweli kwamba, mwanamke anasawiriwa katika hali ya uduni tu katika kazi za fasihi simulizi bali pia zipo kazi zinazomsawiri mwanamke katika hali ya uchanya.

Pia, tunakiri kwamba, usawiri chanya kumhusu mwanamke unaojitokeza katika kazi za fasihi simulizi bado ni ule unaomjenga mwanamke kuwa ni mama wa nyumbani anayeweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Maelezo haya yanatupatia shauku la kutafiti taswira ya mwanamke katika kazi za riwaya ili kupata picha kamili ya maendeleo ya usawiri wa mwanamke katika kazi ya *Utengano*.

Mulokozi (1982) katika makala yake "Protest and Resistance in Swahili Poetry 1660-1885," amezungumzia masuala mengi ikiwemo taswira ya mwanamke. Ameona kuwa ushairi wa Kiswahili uliathiriwa kwa kiasi kikubwa na mfumo wa Kimwinyi, mfumo ambao ulithamini sana anasa, mapambo na kumchukulia mwanamke kama chombo au kitu cha kuondosha hamu ya mwanaume ya kimapenzi. Hivyo, ushairi ulifuata muelekeo huo kwa kumsawiri mwanamke kuwa ni kiumbe duni ambaye anatumiwa na mwanaume kama chombo cha kuburudisha na kutimiza haja ya mapenzi ya mwanaume.

Vilevile, mwanamke amesawiriwa kuwa ni mtumishi, mlezi, asiye na upeo wa mawazo mazuri bali mawazo yake yamefungwa katika kufikiri namna ya kumpendezesha na kumridhisha mwanaume. Maelezo ya Mulokozi (ameshatajwa) yanakabiana na yale ya Matteru (ameshatajwa) kwamba mwanamke ni kiumbe anayesawiriwa kuwa hana upeo wa kuweza kuona mbali na pia ni chanzo cha maovu duniani. Maelezo haya yalitupatia hamu ya kutaka kufahamu maendeleo ya taswira ya mwanamke yamefikia wapi hasa katika kipindi hiki cha utandawazi. Hivi mwanamke bado anaendelea kusawiriwa hivyo hata katika kipindi hiki cha utandawazi? Utafiti huu unakusudia kujibu swali hili pale utakapokamilika.

Kiango (1992) alihakiki taswira ya mwanamke katika baadhi ya tamthilia za Kenya na kugundua kuwa pamoja na kuwa wanawake wana mchango mkubwa katika maendeleo ya jamii, kama vile kushiriki katika ukombozi wa nchi, kilimo na mfanyakazi wa kazi zote za nyumbani. Nafasi aliyopewa mwanamke katika tamthilia hizo inaonesha kwamba bado haijabadilika tangu enzi za akina Mwanakupona (1858) mpaka kufikia leo. Waandishi hao wametoa picha hiyo ya mwanamke bila ya kuangalia hali yake ya kiuchumi na kijamii au mchango wake kihistoria hususani katika kipindi hiki cha utandawazi.

Utafiti huu wa Kiango (ameshatajwa) unaonekana kuwa na mchango muhimu wa kusukuma mbele utafiti wetu kwa kudokeza kwamba usawiri wa mwanamke katika kazi za fasihi bado hautofautiani sana na ule wa "Mwanakupona" licha ya mwanamke wa sasa kuwa katika mfumo tofauti wa maisha na ule wa "Mwanakupona." Mawazo haya tunakubaliana nayo kwa kiasi fulani lakini si kwa asilimia mia moja. Maisha aliyoishi "Mwanakupona" ni maisha tofauti kabisa na maisha ya mwanamke ambaye anaishi katika maisha ya kitandawazi kwa kuwa maisha hayo yanatofautiana. Hata hivyo, katika kulibainisha hili tuliona kuwa kuna haja ya kufanya utafiti wenye lengo la kutafiti taswira ya mwanamke katika riwaya ya *Utengano*.

Mhakiki mwingine ambaye ameshughulika taswira ya mwanamke katika kazi za fasihi ni Wegesa (1994) ambaye alihakiki nafasi ya mwanamke katika tamthilia tano za Ebrahim Hussein ambazo ni *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* (1976), *Alikiona* (1970), *Wakati Ukuta* (1970), *Mashetani* (1971) na *Kwenye Ukungo wa Thimu*

(1988). Katika uhakiki wake anaonesha kuwa nafasi na wajibu wa mwanamke inayojitokeza katika tamthilia za Ebrahim Hussein inafanana na nafasi na wajibu aliopewa mwanamke katika utamaduni wa kijadi. Katika utamaduni huo mwanamke alidunishwa na kuchukua nafasi ya pili baada ya mwanaume. Wegesa (ameshatajwa) anaona kuwa, taswira ya mwanamke katika vitabu hivyo hazichangii katika kumzindua mwanamke juu ya hali yake katika jamii kwani juhudi za baadhi ya wanawake wanaosawiriwa kujikomboa, harakati zao hazifui dafu.

Maelezo ya Wegesa (ameshatajwa) yanatukumbusha kwamba, wanawake wamekuwa katika harakati za kujikomboa kwa kipindi kirefu lakini hawafanikiwi kutokana na kushamiri kwa mfuma dume katika jamii. Maelezo haya tunakubaliana nayo kwa msingi kwamba ni ukweli usiopingika kuwa wanawake wameshindwa kupiga hatua kubwa za maendeleo ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni kutokana na kufungwa katika misingi ya mfumo dume unaotawala katika jamii. Hata hivyo, katika kipindi cha utandawazi misingi ya mfumo dume imelegezwa kwa kiasi kikubwa kutokana na harakati mbalimbali za ukombozi wa mwanamke zilizofanyika kama mvua kuanzia miaka ya 1980 na kuendelea mpaka leo. Kwa hivyo, mwanamke wa sasa ni tofauti kabisa na mwanamke wa kipindi cha kabla ya harakati hizo. Hivyo basi, utafiti tunaokusudia kuufanya unalenga kuchunguza maendeleo ya taswira ya mwanamke katika riwaya ya *Utengano*.

Momanyi (2000) katika makala yake aliyoiita “Nafasi ya Mwanamke katika Ushairi wa Shaaban Robert,” anaonesha namna ushairi wa mwandishi huyo unavyodhihirisha uduni wa mwanamke. Anaeleza kuwa taswira ya mwanamke

katika ushairi huo inamuonesha mwanamke kama ni kifaa cha kumstarehesha mwanaume na huchukuliwa kama pambo au kiumbe asiyeaminika. Hivyo basi, anaona kuwa taswira hii ni miongoni mwa mwendelezo wa maadili ya utamaduni uliomlea mwandishi unayohusishwa na itikadi za kidini.

Kimsingi, mtafiti anakubaliana na mawazo ya Momanyi (ameshatajwa) kuwa utamaduni na itikadi za dini zina mchango mkubwa katika kumsawiri mwanamke kama chombo cha starehe au hali yoyote ile ya uduni. Hata hivyo, ni jambo lililowazi kuwa utamaduni wa jamii hubadilika taratibu kulingana na mabadiliko mbalimbali yanayotokea katika maisha ya jamii (Ngaiza, 2002). Tangu enzi za Shaaban Robert mpaka leo ni miaka mingi imekwishapita na bila shaka yametokea mabadiliko mengi katika nyanja zote za maisha ya jamii. Jambo hili linaashiria kuwa, yapo mabadiliko kadhaa katika taswira ya mwanamke katika kazi za fasihi. Ili kuweza kuthibitisha suala hili tulifanya utafiti wa kuchunguza usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Utengano*.

Naye Mule (2004) alihakiki tamthilia za Kiswahili zilizoandikwa na wanawake kama vile Muhando, Chogo, Ryanga na Mwachofi. Mawazo yake ni pamoja na waandishi hawa kuwa ni wanawake wana mtazamo tofauti katika kumsawiri mwanamke, kwani kuna baadhi yao wamemsawiri mwanamke katika hali ya kumkweza na wengine wamemtweza. Mfano mzuri ni Muhando (1982) katika tamthilia yake ya *Nguzo Mama* anaonekana kumsawiri mwanamke katika hali ya kumkweza na wakati huo huo anamtweza. Hata hivyo, anaona kuwa waandishi wote hawa wanaonekana kuwa na mwelekeo mmoja juu ya kumkomboa mwanamke. Kwa maoni yao, wanaona

kuwa, wanawake na wanaume ni watu wanaotegemeana katika kufanikisha maisha yao ya kila siku, hivyo kuna haja ya kuwepo usawa kati yao ili kuleta ustawi wa maisha kwa kila mmoja pasipo kubugudhiana.

Maelezo ya Mule (ameshatajwa) yanatufanya tujiulize swali kwamba, inakuwaje waandishi wa kike wawasawiri wanawake wenzao katika hali ya uhasi badala ya uchanya? Jibu la swali hili ni kuwa, suala lililowafanya wanawake hawa kumsawiri mwanamke katika hali hiyo si jingine bali ni mfumo dume unaotawala katika jamii. Mfumo dume umemfanya mwanaume kuwa katika tabaka la juu na mwanamke kuwa katika tabaka la chini na hivyo kutazamwa kama chombo cha starehe kwa mwanaume. Kimsingi, kutokana na harakati za kumkomboa mwanamke kufanyika kwa kiwango kikubwa mwanamke amekuwa kinara katika ushiriki wa masuala mbalimbali ambayo hapo nyuma yalionekana kuwa ni ya mwanaume. Mabadiliko haya yanatufanya tufanye utafiti wa kina katika kutazama ni kwa vipi riwaya ya Kiswahili nayo imeenda sambamba na mabadiliko haya na hivyo kumsawiri mwanamke katika taswira inayoendana na mabadiliko hayo. Lengo hili litafanikiwa kwa kutafiti usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Utengano*.

Omari (2008) katika makala yake ‘Fasihi Simulizi na Jinsia,’ amechunguza namna mtoto wa kike na kiume wanavyochorwa na kushirikishwa katika nyimbo za watoto za Tanzania. Anaona kuwa, nyimbo hizo zimemsawiri mwanamke kuwa hana sauti kwa mume wake, mzalishaji mali na kiungo muhimu cha malezi ya familia. Mwanaume kwa upande mwingine anaonekana kuwa ndie mwenye kumiliki mali katika familia, mwenye sauti na mwenye mamlaka makubwa katika jamii. Aidha,

ujinsia umejitokeza katika mgawanyo wa majukumu ya mtoto wa kike na kiume katika michezo yao. Kwa mfano, huwa kuna michezo ya watoto wa kiume kama vile kuendesha gari, na kwa upande wa watoto wa kike ni kupika na kubeba mtoto. Kutokana na hali hiyo nyimbo hizo zinawajenga watoto kiakili na kimatendo tangu wakiwa wadogo kwamba majukumu ya mwanamke na mwanaume ni yapi na ni vigumu kubadilika kirahisi wawapo watu wazima.

Mawazo haya tunakubaliana nayo na tunaungana nayo mkono kwa asilimia mia kwa mia kwa kuwa yana mashiko yanayoweza kuaminiwa kitaaluma. Hata hivyo, ni dhahiri kwamba, michezo ya watoto ya siku hizi imebadilika kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na ile ya wakati wa zamani jambo ambalo litakuwa limesawiriwa na kazi mbalimbali za fasihi za kipindi hiki. Utafiti uliofanywa umeonesha ni kwa vipi taswira ya mwanamke imepata maendeleo kupitia riwaya ya *Utengano*.

Naye mwanataalimu anayejulikana kwa jina la Philip (2009) alifanya utafiti ulioangalia namna matumizi ya lugha katika taarab ya mipasho na bongo fleva yalivyomchora mwanamke. Kwa upande wake amegundua kuwa nyimbo hizo zimejaa hali ya ujinsi ambapo taarab ya mipasho imeonesha ujinsia wa hali ya juu kuliko bongo fleva. Philip anaeleza kuwa taarab ya mipasho inamsawiri mwanamke katika hali ya udhalilishwaji na kumfanya ajikubalishe mwenyewe kuwa ni kiumbe duni kuliko mwanaume. Mwanamke katika taarab hiyo hujinadi, hujisifu na hushindana dhidi ya wanawake wenzake juu ya namna anavyoweza kumfurahisha na kumstarehesha mwanaume, jambo ambalo ni kinyume katika nyimbo za bongo fleva.

Mawazo ya Philip (ameshatajwa) yanaonesha kwamba mabadiliko katika jamii yanamchango mkubwa katika kujenga dhamira na maudhui ya kazi za fasihi. Muziki wa Kizazi Kipya umeibuka kutokana na mabadiliko katika jamii yaliyoletwa na utandawazi na ukaweza kwa kiasi fulani kumsawiri mwanamke katika hali ambayo si ya uduni sana kama ilivyo katika nyimbo za taarab hasa ile ya mipasho. Uhalisia huu wa usawiri wa mwanamke unajitokeza pia katika riwaya ya Kiswahili na hivyo kutusukuma kufanya utafiti wa kina ili kuweza kuona ni namna gani usawiri wa taswira ya mwanamke umepiga hatua katika utanzu huu wa fasihi andishi ya Kiswahili. Tumetimiza lengo hili kwa kuchunguza taswira ya mwanamke katika riwaya ya *Utengano*.

Mnenuka (2011) amechunguza nafasi na hadhi ya mwanamke katika jamii kama inavyojadiliwa katika nyimbo za Bongo Fleva za *Dege*, *Samaki* na *Bata* zilizoimbwa na Offside Trick na *Vocha* iliyoimbwa na Hassan Kumbi na Ashlay. Anaeleza kuwa, uhusiano wa kingono baina ya mwanamke na mwanaume, sambamba na hadhi na nafasi zao katika uhusiano huo umetokana na malezi ya kijamii. Katika jamii mwanamke anapaswa kuwa mtulivu, ilhali mwanaume anapaswa kuwa mtendaji mkuu na mwenye kutoa sehemu kubwa ya uamuzi katika masuala mengi. Hivyo taswira ya mwanamke inayopatikana katika misemo na nyimbo za kazi nyingi za kifasihi zinaonesha udogo wa mwanamke kama ulivyo katika jamii nyingi. Kwa mfano katika nyimbo teule za bongo fleva taswira ya mwanamke inayoonekana ni chombo cha starehe cha mwanaume hasa kingono na thamani yake hushuka mara tu anapomaliza kukutana na mwanaume kimwili na kuwa kiumbe asiyefaa katika jamii.

Mawazo ya Mnenuka (ameshatajwa) yanatupatia mwanga wa kuelewa kwamba, taswira ya mwanamke kama chombo cha starehe kwa mwanaume bado inaendelea kusawiriwa katika kazi za fasihi. Katika utafiti wetu tumechunguza ni kwa vipi hali hiyo inajitokeza katika riwaya ya *Utengano*.

2.3 Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya za Kiswahili

Mbughuni (1982) alichunguza juu ya usawiri wa mwanamke katika riwaya za Kiswahili za Tanzania. Katika uchunguzi wake anaeleza kuwa mwanamke katika riwaya hizo husawiriwa katika sura mbili. Sura ya kwanza ni ile inayotokana na kisa cha Eva kama ni mshawishi aliyetumia ulaghai wa kingono na kusababisha Adamu kufanya maovu na hatimaye kutolewa peponi. Hivyo wanawake katika riwaya za Kiswahili huchorwa kama ni vishawishi wanaosababisha wanaume kufanya maovu kama vile kuiba, kuua, kulewa, kufanya ngono au kutelekeza familia zao. Hali hii hupelekea wanaume hao ama kuanguka kimaisha, kufungwa, kuuawa au kuhasimiana na ukoo au familia zao. Katika taswira hii mwanamke anaonekana kuwa ni chanzo cha maovu yote yanayotokea katika jamii. Hivi ndivyo mwanamke anavyosawiriwa katika riwaya nyingi za wakati uliopita jambo ambalo limetusukuma kufanya utafiti wa kina kwa nia ya kutazama usawiri wa mwanamke katika riwaya za Kiswahili. Tumetimiza lengo hili kwa kutumia riwaya ya *Utengano*.

Maelezo ya Mbughuni (ameshatajwa) yanatupatia mwanga wa kufahamu namna mwanamke anavyosawiriwa katika kazi za fasihi ili nasi tuweze kuhusianisha na utafiti wetu. Utafiti tulioufanya ulilenga kubainisha usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Utengano*.

Naye mwandishi makini katika fasihi ya Kiswahihili, Khatib (1986) alifanya uchambuzi wa riwaya ya *Kuli*, katika uchambuzi huo anaeleza kuwa, wanawake katika riwaya hiyo wanapewa nafasi yao katika harakati za ukombozi badala ya kugeuzwa kuwa ni chombo cha anasa na starehe-wanawake wamechorwa wakiwa ni wanamapinduzi. Akitoa mfano, Khatib (ameeleza) anaeleza kuwa katika mgomo wa makuli, wanawake walijitolea kutoa chakula bure ili kuwahudumia makuli waliogoma kufanyakazi bandarini Zanzibar. Aidha, mwandishi anawachora wanawake wakiwa na mawazo mazuri katika kuendeleza shughuli hizo za ukombozi. Kwa mfano, anawaonesha wanawake wakifanikisha kufikisha ujumbe wa kugoma ulioandikwa katika karatasi kwa makuli na watu wengine katika jamii.

Kwa mtazamo wetu mwandishi huyu anajaribu kutuonesha kwamba mwanamke ni mtu anayeweza kufanya mambo yanayofanywa mwanaume kama kuchangia mawazo ya kimaendeleo. Mawazo ya Khatib (ameshatajwa) yanatupatia ufahamu kwamba, mwanamke ni kiumbe shupavu anayeweza kuleta mabadiliko ya kimaendeleo katika jamii. Mawazo haya yanakinzana na kazi nyingi za fasihi ambazo kwa kiasi kikubwa humsawiri mwanamke kama chombo cha starehe kwa mwanaume.

Pamoja na kukinzana na kazi nyingine za fasihi kuhusu taswira ya mwanamke na kumuonesha mwanamke kama mwanaharakati wa kimapinduzi lakini bado Khatibu (ameshatajwa) anamuonesha mwanamke kama mama wa nyumbani na kwamba shughuli za kumpikia mwanamme ndio kazi yake kuu. Haya yanajionesha pale anaposema kwamba wanawake walipigania ukombozi kwa kuwapatia chakula makuli waliokuwa katika mgomo wa kuleta ukombozi.

Kimsingi, Kitendo cha wanawake kutoa chakula bure kwa makuli hao kianaonesha kwamba wanawake hao nao walikuwa ni wanaharakati na wameshiriki kikamilifu katika harakati hizo. Suala hili hatulipingi hata kidogo ila tunaona kwamba, bado usawiri huu unamtaja mwanamke kama chombo cha kumhudumia mwanaume na kwamba mahali stahili kwa mwanamke huyu ni nyumbani. Mawazo haya yalitupeleka mbali zaidi katika kuchunguza ni upi usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Utengano*?

Si hivyo tu, bali pia, Lyatuu (2011) alichunguza tofauti za usawiri wa mwanamke katika riwaya zilizoandikwa na waandishi wa kike ambao ni Balisidya (1981) na Mwanga (1984) na riwaya zilizoandikwa na waandishi wa kiume ambao ni Kezilahabi (1971) na Mohamed (1976). Katika utafiti wake alibaini kuwa waandishi wa kike pia wameshiriki katika kumsawiri mwanamke katika hali duni, dhaifu na yenye udhalilishaji. Kwa mfano, wamemchora mwanamke kama kiumbe laghai, fuska na mwenye kukosa maadili. Pia wamemchora kama kiumbe asieye na ruhusa ya kumiliki mali ila kuzitafuta na kuzilinda kwa ajili ya mwanaume. Hata hivyo, wakati mwingine wamemsawiri kama ni mpole, mnyenyekevu na mstahamilivu.

Maelezo ya Lyatuu (2011) yana mashiko na ukweli ambao unakubalika na kuaminika katika ulimwengu wa taaluma zinazohusiana na masuala ya kijinsia. Ni dhahiri kwamba, waandishi wanawake aliowataja wamemsawiri mwanamke katika hali hiyo si kwa sababu wanapenda kumuona mwanamke katika hali hiyo bali mfumo dume unaotawala maisha ndio uliowalazimisha kumsawiri mwanamke katika hali hizo. Hata hivyo, katika kipindi tulichonacho cha utandawazi yapo masuala

ambayo yamejitokeza hasa yale yanayohusu harakati za ukombozi wa mwanamke na kupunguza kasi ya mfumo dume katika jamii. Mabadilko haya yamemfanya mwanamke kuonekana katika taswira ambazo ni tofauti na zile zilizokuwa hapo awali. Ufahamu na uelewa huu ulitusukuma katika kuchunguza ni upi usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Utengano*.

Shivji (2002) alifanya mapitio ya riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria* na kuwasilisha mapitio hayo katika uzinduzi wa riwaya hiyo. Katika mapitio yake anasema riwaya ya hii ni muhimu katika kuendeleza harakati za mapambano ya wanyonge dhidi ya mifumo kandamizi. Bila shaka wanyonge wanaotajwa katika riwaya hii wanajumuisha kundi la wanawake pamoja na makundi mengine. Ingawa halikuwa lengo la Shivji (ameshatajwa) kuchambua riwaya hii kifasihi, lakini ametupatia mwanga wa kuyafahamu mambo kadhaa ambayo yatatusaidia katika utafiti wetu. Jambo kubwa alilotusaidia kulifahamu ni msingi wa kinadharia ambao tunaweza kuutumia katika kuhakiki na kutafiti riwaya ya *Utengano*. Msingi huo si mwingine bali ni ule unaohusu uchambuzi wa kitabaka ambapo kupitia matabaka yaliyopo katika riwaya hii tumeupata usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Utengano*.

Mbonde (2004) alifanya uchambuzi wa riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria* kwa kutazama vipengele vya dhamira, muundo na mtindo. Katika uchambuzi wake anasema kwamba, dhamira inayotawala katika riwaya ya *Makuadi wa soko Huria* ni suala la ukombozi wa kitabaka. Kwa upande wa muundo na mtindo, anasema kwamba, mtunzi anatumia mbinu rejeshi; anachanganya usimulizi na uandishi ili kuileta hadhira karibu na msimuliaji. Kimsingi, uchambuzi huu uliofanywa na

Mbonde (ametajwa) ni muhimu katika kusukuma mbele utafiti wetu kwa namna kadhaa. Kwanza, umetufahamisha kwamba dhamira iliyotawala ni ile ya ukombozi wa kitabaka na bila shaka mwanamke ni miongoni mwa watu walio katika harakati za kujikomboa. Kwa hiyo, katika utafiti wetu tumeweza kuainisha namna mwanamke anavyosawiriwa katika harakati hizo.

Mulokozi (2012) ameihakiki riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria* katika muktadha wa riwaya ya Kiswahili ya Kihistoria. Katika makala yake Mulokozi (ametajwa) anaeleza kuwa riwaya hii ya Chachage ni miongoni mwa riwaya bora kabisa katika riwaya za Kiswahili ambayo inashughulikia migogoro ya kitabaka katika jamii. Anasema kwamba, matabaka yaliyopo katika jamii inayosawiriwa katika riwaya hiyo ni yale ya wananchi masikini na wale matajiri ambao wanafurahia mfumo wa Ubepari ambao ni nyonyaji na kandamizi kwa wananchi masikini.

Makala ya Mulokozi (ameshatajwa) yanatoa mchango madhubuti wa kusukuma mbele utafiti wetu kutokana na kudokeza kwake mfumo wa Ubepari. Mfumo huu kwa hakika huelekeza jamii kuwa wabinafsi na wasiowajali wanadamu wenzao. Kuwepo kwa mfumo dume katika jamii za Afrika kumemfanya mwanamke kuwa ni tabaka la chini katika kila sekta ya maendeleo katia nchi nyingi za Afrika.

Kwa msingi huu, kuwepo kwa ubepari ambao nao unahimiza ubinafsi miongoni mwa wanadamu ni pigo kubwa kwa harakati za ukombozi wa mwanamke ambaye tayari yupo katika tabaka la chini. Utafiti wetu unafanywa ili kubainisha namna mwanamke anavyosawiriwa katika riwaya ya *Utengano*.

2.4 Mkabala Wa Kinadharia

2.4.1 Utangulizi

Nadharia ni muongozo ulioandaliwa kwa ajili ya kuwezesha shughuli fulani kufanikiwa kama ilivyokusudiwa. Kwa mfano, katika kufanya utafiti wa kitaaluma ni wajibu kwa mtafiti kuongozwa na nadharia maalumu katika kufanya utafiti wake ili kuufanya ufanikiwe vizuri na uaminike. Utafiti huu umeongozwa kwa nadharia ya Ufeministi. Maelezo kwa kila nadharia yanatolewa hapa chini kama ifuatavyo:

2.4.2 Nadharia ya Ufeministi

Katika utafiti huu pia tumetumia nadharia ya ufeministi ambayo ilituongoza katika uchambuzi na uwasilishaji wa data kwa kuzingatia misingi yake. Kwa mujibu wa Bouchier (1983) ufeministi ni dhana inayoelezea hali na tendo la wanawake wanaodai kujieleza katika jamii mbalimbali na wanaume wanaounga mkono jitihada za wanawake hao. Ni dhana inayopinga mfumo dume na kujaribu kutatua matatizo yanayowakabili wanawake katika jamii ambazo zinaongozwa na mfumo dume katika maisha yake ya kila siku.

Mackinnon (1991) anaeleza kuwa nadharia ya Kifeministi ilianza mwanzoni mwa miaka ya 1792 huko Ulaya, hususani katika nchi za Uingereza na Marekani. Katika kipindi hicho wanawake hawakuthaminiwa katika jamii zao na walikuwa ni watu waliokuwa katika daraja la chini. Vilevile, wanawake hawakuhusishwa katika shughuli mbalimbali za kijamii, kisiasa na kiuchumi kama vile kupiga kura au kuchaguliwa katika uongozi, kumiliki mali, kupata elimu, kuajiriwa na kadhalika. Mwanamke alionekana kama kiumbe anayestahili kufanya kazi za jikoni na za

nyumbani kwa ujumla. Kazi zake ni kama vile kupika, kuosha vyombo, kufua nguo za familia nzima, kusafisha nyumba na kuhudumia pamoja na kulea watoto (Moore, 1998). Kwa mujibu wa Moore (ameshatajwa) anaiona hali hii kuwa ni unyanyasaji dhidi ya mwanamke kwa msingi huo ndipo nadharia ya ufeminist ikaibuka.

Nadharia ya kifeministi ilianza kuzungumzwa katika karne ya 19 na kushika kasi katika miaka ya 1960 na 1970 (Odim, 1991). Katika kipindi hiki Wanawake wa nchi za Magharibi yaani Marekani na mataifa ya Ulaya walianza kuzungumzia matatizo yanayowakabili wananchi wa tabaka la chini wakiwemo wanawake. Matatizo hayo yalikuwa ni ya kiuchumi, kisiasa na kijamii (Wafula na Njogu 2007).

Wamitila (2002) anaeleza kuwa baadhi ya kazi za mwanzo kuyafafanua masuala ya wanawake kinadharia ni *A Vindization of the right of a woman* (1792) ya Mary Wollstonecraft. Pia kazi nyingine ni *The Second Sex* (1952) ya Simone de Beauvior ambaye alikosoa na kushambulia baadhi ya asasi zinazochangia katika kumdhalilisha au kumdunisha mwanamke, kama vile dini, ndoa na utamaduni. Kwa mujibu wa Wamitila, Simone de Beauvior anaeleza kuwa utamaduni anamokulia mwanamke unachangia katika kumdidimiza katika hali ya unyonge. Utamaduni huo unamfanya na kumlazimisha kukubali kuwa yeye ni kiumbe duni. Baada ya kukubali hali hiyo, mwanamke anaishia kuwa chombo cha mfumo wa jamii cha kuendeleza utamaduni huo. Mfano, ndoa ni asasi mojawapo ya kiutamaduni inayoendeleza ukandamizaji wa wanawake ambayo inamjenga kwenye imani na uwezo mkubwa alionao mwanaume na kuishia kumuangalia mwanamke kama chombo tu hasa cha starehe.

Wamitila (2002) anandelea kueleza kuwa uhakiki wa kifeministi wa Kimarekani

unahusishwa na kazi ya Mary Ellman, *Thinking about Woman*. Dhamira ya kimsingi ya mwandishi huyu ilikuwa ni kuangaza jinsi wanawake walivyosawiriwa kwa namna mbali mbali katika kazi zilizoandikwa na wanaume. Mwandishi huyu alimulika pia jinsi baadhi ya waandishi wa kike walivyouendeleza usawiri huo hasi wa wanawake katika kazi zao. Hali hii ilitokana na wao kukulia kwenye jamii zilizotawaliwa na itikadi ya kiume au "ubabedume" na kuishia kufyonza baadhi ya mitazamo kumhusu mwanamke ambayo inaakisiwa kwenye kazi zao.

Ntarangwi (2004) anasema kuwa nadharia ya kifeministi ni siasa kutokana na ukweli kwamba inaelekeza kubadili uhusiano uliopo kati ya wanaume na wanawake. Uhusiano ambao umeranda katika nyanda nyingi za maisha kama vile familia, elimu, kazi, siasa, utamaduni na hata mambo ya starehe na anasa. Hivyo basi, ni nadharia inayotaka kuelekeza wanajamii namna ya kuishi, kutenda, na jinsi watakavyokuwa siku za usoni.

Kwa upande wa fasihi Ntarangwi (keshatajwa) anasema kuwa nadharia ya ufeministi imekuja kwa azma ya kusoma upya kazi za fasihi ili kusisitiza vipengele vilivyopuuzwa na wahakiki wengi ambavyo hawangeviona kwa sababu walikuwa wanafanya kazi katika nadharia za kijadi zilizomtukuza mwanaume.

Ntaragwi (2004) anaeleza kuwa baadhi ya mambo yanayozungumzwa na muungano huu ni kuunda upya uhalisia wa mwanamke kwa kupanga na kudhihirisha miundo ya kijadi ambayo inamtukuza mwanaume na kumkandamiza mwanamke. Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007) nadharia ya kifeministi inaongozwa na misingi kadhaa,

nayo ni kutumia fasihi kama jukwaa la kuelezea kwa uyakinifu hali ya mwanamke, kusawazisha wanadamu kwa upande wa utamaduni na kupigania jamii mpya yenye msingi katika amali za kibinadamu. Misingi mingine ni kuhamasisha utungaji wa kazi za kisanaa zenye wahusika wa kike wanaoweza kuigwa ambao hawategemei wanaume ili wajulikane, huzindua mwamko kwa upande wa wanawake jinsi wanavyojiona na huvumbua na kuziweka wazi kazi za fasihi zilizotungwa na wanawake.

Kimsingi, nadharia ya Kifeministi inegawanyika katika makundi kadhaa: Miongoni mwa makundi hayo ni “Radical Feminism”, “Marxist Feminism”, “Cultural Feminism” na “Political Feminism” (Macknnon, 1991). Tukianza na kundi la kwanza ambalo ni Radical Feminism (Wanaufeministi wenye msimamo mkali) wao wanadai kwamba, ndoa ndio ya taasisi ya kwanza inayohusika katika kunyanyasa na kumnyonya mwanamke. Ni katika ndoa ndipo mwanamke anafanywa kuwa chombo cha starehe na mtumishi wa mwanaume pasipo malipo huku mwanaume akienda kazini na kulipwa mshahara. Kwa maoni yao ili haki sawa ipatikane baina ya mwanamke na mwanaume basi ni lazima mwanamke aache uhusiano na mwanaume (Eisenstein, 1979). Kwa maneno mengine suala la ndoa kati ya mwanamke na mwanaume lisiwepo na kama mwanamke anahitaji mototo atumie uzazi wa chupa.

Kwa upande wa Marxist Feminism (Wanaufeministi wa Kimarx) wanadai kwamba jamii imeundwa kwa matabaka mawili, tabaka la walionacho na lile la wasionacho. Wanawake waliowengi wanaingia katika tabaka la wasionacho kutokana na mfumo dume uliotawala katika jamii. Njia pekee ya kuwaokoa wanawake kutoka katika

mfumo huu ni serikali kuingilia kati na kuundesha uchumi pamoja na kutoa huduma muhimu kwa watu wote. Sekta binafsi ikiachwa itoe huduma hizo ni wazi kwamba mwanamke ataendelea kuwa duni (Eisenstein, 1979).

Cultural Feminism (Wanaufeministi wa Kiutamaduni) kwa upande wao wanadai kwamba, suala la mwanamke kujipamba na kujipodoa ni la asili na ni haki ya mwanamke kufanya hivyo (Leacock, 1981). Haki hii ya mwanamke isije ikachukuliwa kama ni sababu ya kumuona mwanamke kama chombo cha kumstarehesha mwanaume na hivyo kumgandamiza mwanamke.

Kwa upande wa Political Feminism (Wanaufeministi wa Kisiasa) wao wanadai kwamba wanaume ndio waliotawala katika nafasi mbalimbali za uongozi huku mwanamke akiachwa nyuma katika hili. Kutokana na hali hii masuala ya wanawake pamoja na haki zao hayazungumzwi na kuundiwa mikakati matdhubuti ikilinganishwa na yale yanayowahusu wanaume (Leacock, 1981). Kwa mantiki hiyo basi ni lazima wanawake washirikishwe katika uongozi kwa kupewa nafasi sawa na wanaume ndiyo masuala ya wanawake yatapewa kipaumbele katika miradi mbalimbali ya maendeleo.

Kimsingi, makundi yote haya yanaijenga natharia ya ufeministi kuonekana kwamba ni imara katika kutatua matatizo ya wanawake na kuleta usawa katika jamii. Natharia hii inatusaidia kuelewa kwamba mwanamke si chombo cha starehe kwa mwanaume kwani wote ni wanaadamu na wanapaswa kuwa na hadhi iliyosawa katika jamii. Ubora mwingine wa nadharia hii ni kwamba imeweza kuainisha sababu mbalimbali

zinazofanya mwanamke aonekane kiumbe duni katika jamii. Sababu kubwa kuliko zote ni kwamba, mfumo dume uliotawala katika jamii ndio uliosababisha mwanamke kutazamwa kama kiumbe duni. Katika utafiti huu tumechunguza taswira ya mwanamke katika riwaya ya *Utengano* ili kuona ni namna gani mwanamke anasawiriwa katika riwaya hii ikuhusianishwa na mfumo dume.

2.5 Hitimisho

Sura ya pili ya tasinifu hii imepitia kazi za watafiti na wahakiki watangulizi kwa lengo la kubaini ni kitu gani ambacho tayari kimefanyika na nini bado. Kwa jumla, tumebaini kuwa zipo kazi tangulizi ambazo zimechunguza taswira ya mwanamke katika riwaya teule lakini hakuna mtaalamu aliyeitafiti riwaya ya *Utengano* ya Said Ahmed Mohamed. Hivyo, tukaona kuwa ni jambo zuri nasi tuchunguze usawiri wa mwanamke katika riwaya hii ili kuona ina tofauti gani na riwaya ambazo tayari zimeshatafitiwa.

SURA YA TATU

3.1 MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Mbinu za utafiti ni taratibu, kanuni au sheria ambazo zinapaswa kutolewa ili kufuatwa katika hatua zote za utafiti wa kitaaluma ili kuufanya utafiti huu uweze kuaminiwa kitaaluma. Katika utafiti huu tumekusanya data za maktabani na kutoka katika riwaya iliyoteuliwa. Yafuatayo ni maelezo kamili juu ya kila mbinu za utafiti zilizotumika pamoja na sababu za kuteua mbinu kila mbinu.

3.2 Eneo la Utafiti

Kothari (2008) anaeleza kwamba, eneo la utafiti ni mahali ambapo utafiti husika unapofanyikia. Ukubwa ama udogo wa eneo lenyewe hutegemea nia ya utafiti husika kwamba unataka kutimiza jambo gani. Utafiti huu ulifanyika katika jiji la Dar es Salaam ambapo maktaba za Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu Huria ndipo zinapopatikana. Huu ni utafiti wa maktabani na hivyo maktaba zilizotajwa ni muafaka katika kufanikisha utafiti wetu.

3.3 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni mpangilio maalumu unaotoa mchoro kamili juu ya namna au jinsi utafiti fulani ulivyofanyika tangu hatua za mwanzo kabisa mpaka kukamilika kwake (Babbie, 1999). Kwa maana hiyo basi zipo aina mbalimbali za usanifu wa utafiti na kwa minajili ya utafiti wetu tumeteua uchunguzi kifani kuwa sehemu ya utafiti huu. Uchunguzi kifani ni aina ya usanifu wa utafiti ambapo mtafiti huteua

sehemu tu, ya watafitiwa au vitafitiwa vilivyovingi kwa ajili ya kuvifanyia utafiti ambavyo bila shaka hutoa uwakilisho wa watafitiwa au vitafitiwa vyote. Katika utafiti huu tumeteua riwaya ya *Utengano* kwa sababu hatukuwa na muda wa kutosha kutafiti kazi za waandishi wengi wa riwaya. Kothari (2008) anaeleza kwamba, uchunguzi kifani ni aina bora ya usanifu kwa sababu humfanya mtafiti kutumia muda mfupi na gharama nafuu katika kupata data za utafiti na kisha kukamilisha malengo ya utafiti wake.

3.4 Aina ya Data Zilizokusanywa

Katika utafiti huu zimekusanywa data za aina mbili zikihusisha data za msingi na za upili. Maelezo kamili juu ya data hizo yanatolewa hapa chini kama ifuatavyo:

3.1.1 Data za Msingi

Kwa mujibu wa Yin (1994) anaeleza kwamba, data za msingi ni aina ya data za utafiti ambazo hukusanywa kwa mara ya kwanza na hazijawahi kukusanywa na watafiti wengine kwa nia ile ile aliyokuwa nayo mtafiti husika, yaani mtafiti huyu aliyefanya utafiti sasa hivi. Hivyo basi, data za msingi za utafiti huu zilikusanywa kutoka katika riwaya teule ya *Utengano*.

3.1.2 Data za Upili

Tofauti na data za msingi, data za upili ni aina ya data ambazo tayari zilishakusanywa na watafiti wengine na kukamilisha tafiti zao. Mtafiti huenda katika maktaba kwa lengo la kukusanya data hizi kwa kupitia na kusoma machapisho kama vile tasinifu, majarida, vitabu na makala mbalimbali. Data hizi hutumika katika

kujazilizia data za msingi ili ziweze kuimarika na kutimiza madhumuni ya utafiti husika. Data za upili zilikusanywa katika maktaba za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

3.2 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Kama tulivyokwisha eleza tangu awali kuwa katika utafiti huu tumekusanya data za aina mbili, yaani data za msingi na upili. Data za msingi zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na data za upili zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya upitiaji wa nyaraka.

3.2.1 Usomaji Makini

Usomaji makini ni mbinu ya kukusanya data za msingi kwa mtafiti kusoma kwa makini kazi alizoziteua na kunukuu yale anayoyataka katika daftari maalumu pale anapokutana nayo (Kothari, 2008). Katika utafiti huu tumekusanya data za msingi kwa kusoma riwaya za waandishi husika na pale tu, tulipokutana na aya, sentensi au neno ambalo linahusiana na malengo yetu ya utafiti tulinukuu katika daftari maalumu tulilolianadaa. Kimsingi, ili kuifanya mbinu hii kuwa na manufaa ya kuwezesha kupatikana kwa data sahihi tuliandaa mada kuu na ndogondogo ambazo ndio tulizitafutia data kutoka katika riwaya husika. Hii ilisaidia kuifanya mbinu hii kuwa fanisi na yenye tija katika kukamilisha madhumuni ya utafiti wetu.

3.2.2 Upitiaji wa Nyaraka

Hii ni mbinu ya ukusanyaji wa data za upili ambapo mtafiti hulazimika kutafuta machapisho mbalimbali yanayohusiana na utafiti wake ili aweze kupata data za

kujazilishia yale aliyoyapata katika data za msingi (Babbie, 1999). Hivyo basi, kupitia mbinu hii tumepitia vitabu, makala, tasinifu, wavuti, tovuti na majarida mbalimbali yanayohusiana na mada yetu ya utafiti ili kupata data ambazo zimesaidia kukamilisha data za msingi na hatimaye kukamilika kwa madhumuni ya utafiti wetu.

3.3 Sampuli na Usampulishaji

Sampuli ni kundi dogo linaloteuliwa kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kupata taarifa zinazohusu kundi kubwa. Sampuli katika utafiti huteuliwa kwa sababu mtafiti hawezi kutafiti watafitiwa wote katika jamii kwa sababu ni suala ambalo ni ghali sana na litachukua muda mrefu kukamilika (Kothari, 2008). Sampuli ya utafiti huu ni riwaya moja tu, ya *Utengano*.

Kwa upande wa usampulishaji, tulitumia sampuli lengwa katika kuteua riwaya ya *Utengano*. Sampuli lengwa ni aina ya sampuli ambapo mtafiti huteua mtafitiwa kwa kuamini kwamba mtafitiwa huyo atampatia data anazozihitaji ili kukamilisha madhumuni ya utafiti wake. Vitabu tulivyoviteua ni muafaka katika kutupatia data tunazozihitaji kwa ajili ya kukamilisha malengo ya utafiti wetu.

3.4 Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data ni kitendo cha kuzipangilia data na kuzitolea maelezo yanayostahili kwa namna ambayo inajibu maswali ya utafiti. Katika utafiti huu tumetumia mbinu ya uchambuzi wa data ya kimaelezo pasipo kuhusisha mahesabu (Robson, 2007). Kwa kutumia mkabala huu, data zilizokusanywa zilipangiliwa vizuri kulingana na mada kuu na ndogondogo ambazo zilibuniwa kwa kuzingatia

madhumuni mahususi ya utafiti wetu. Baada ya hapo, data hizo zilianza kutolewa maelezo ya kiuchambuzi yenye mwelekeo wa kujibu maswali ya utafiti wetu.

3.5 Hitimisho

Sura hii ya mbinu za utafiti imekamilisha lengo lake kwa kutubainishia mbinu za kukusanya na baadaye kuchambua data za utafiti. Mbinu hizo ni eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, sampuli na usampulishaji, aina ya data zilizokusanywa, mbinu za kukusanya na kuchambua data.

SURA YA NNE

3.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

4.1 Utangulizi

Mada ya tasinifu hii ni kuchunguza usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Utengano* iliyoandikwa na Said Ahmed Mohamed. Data za utafiti zimewasilishwa na kuchambuliwa kwa mujibu wa malengo ya utafiti. Malengo mahususi ya utafiti huu yalikuwa mawili ambayo ni kuchambua taswira ya mwanamke katika riwaya ya *Utengano* na kuelezea uhalisia wa taswira ya mwanamke katika riwaya ya *Utengano* kwa jamii ya leo. Uwasilishaji huo wa data ni kama ifuatavyo:

4.2 Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya Utengano

Mwanamke husawiriwa kwa namna tofautitofauti katika kazi za fasihi huku baadhi ya watunzi wakimsawiri mwanamke katika hali hasi na wengine wakimsawiri katika hali chanya. Usawiri hasi juu ya mwanamke unafanywa kwa makusudi kutokana na mfumo dume ambao upo katika jamii ambao humuona mwanamke kama mkosaji kwa kila kitu au jambo lolote katika maisha. Mfumo dume humuona mwanamke kama kiumbe asiyeweza kuwa na maamuzi sahihi ya kufanya jambo bila ya kusaidiwa na mwanaume. Athari hii inajitokeza katika kazi nyingi za fasihi ingawa hivi karibuni kumekuwa na jitihada za kuiondoa mtazamo wa mfumo dume dhidi ya mwanamke.

Riwaya ya *Utengano* ni miongoni mwa kazi za fasihi ambazo zinamsawiri mwanamke katika nafasi mbalimbali kama ilivyowasilishwa katika sehemu hii.

4.2.1 Mwanamke Kiumbe Tegemezi

Mwanamke anasawiriwa kama kiumbe tegemezi kwa mwanaume katika mambo mbalimbali ya maisha. Dhana hii imekuwa ikizunguka katika akili ya baadhi ya wanawake hata wanashindwa kufanya maamuzi muhimu katika maisha yao. Mwandishi katika Utengano ameisawiri hali hii pale anaposema:

> *Pili, anaichukia nafsi yake-nafsi iliyolemaa na kuridhi siku zote kumpembejea mwanaume ambaye ni kiumbe kama yeye. Anachukia hali yake, anachukia jamii yake, anachukia, anachukia kila kitu, kila kitu*… (uk. 01).

Maneno haya yanaonyesha bayana kuwa katika jamii kuna hali ya mwanamke kumtegemea mwanaume katika mambo mbalimbali. Dondoo linaonyesha Kazija ambaye ni mhusika katika riwaya ya Utengano kutoridhishwa na utegemezi wa wanawake kwa wanaume hali ya kuwa mwanaume ni kiumbe kama alivyo mwanamke. Hii inatokana na wanaume kuwa na fursa zaidi za elimu, uchumi, siasa na kumiliki mali huku mwanamke akiwa ni mama wa nyumbani ambaye hana umiliki wa chochote zaidi ya nguo aliyoivaa mwilini mwake kwa wakati huo. Hali hii ndiyo inayowafanya wanawake kuwa wategemezi wa wanaume kwa kila kitu katika maisha. Kama mwanamke angekuwa na uwezo wa kumiliki rasilimali kama ilivyo mwanaume angeweza kuanzisha miradi yake na kupata kipato cha kutosha kujitegemea.

Hata hivyo, maneno katika dondoo hapo juu yanabainisha kuwa wanajamii wanawake hawakubaliani na hali hii ya kumtegemea mwanaume na wapo tayari kujitegemea wao wenyewe pale tu mfumo dume utakapowapa nafasi ya kufanya hivyo. Hii ni hatua nzuri ya kuleta mabadiliko katika jamii na hivi ndivyo nadharia

ya Ufeministi inavyotaka mambo yawe. Wanaufeministi wanaeleza kuwa mwanamke ni kiumbe mwenye uwezo wa akili na maarifa kama ilivyo kwa mwanaume na kwamba mwanamke akiwezeshwa anaweza kufanya vizuri kuliko hata mwanaume (Macknnon, 1991). Maelezo haya yana uhalisia katika maisha ya kila siku ya jamii ambapo tumeshuhudia kundi kubwa la wanawake wakijishughulisha katika shughuli za ujasiriamali na wakifanya vizuri sana. Hii ni nzuri kwa sababu mwanamke anapopata kipato cha kutosha husaidiana na mumewe katika kukidhi mahitaji ya familia. Zipo pia baadhi ya familia ambazo huwa na mama tu bila ya baba lakini akina mama hao wafanya kazi za ujasiriamali na kupata kipato cha kulelea wato wao.

4.2.2 Mwanamke ni Mpenda Starehe

Suala la mwanamke kusawiriwa kama kiumbe ambaye anapenda sana starehe linajitokeza katika kazi nyingi za fasihi ya Kiswahili. Mwanamke anaonekana kuwa ni kiumbe ambaye anapenda kupata starehe kwa gharama za wanaume na si zake yeye binafsi. Jambo ambalo huwa tunajiuliza ni kuwa, hivi mwanamke huwa anafanya starehe yeye peke yake au kwa kushirikiana na wanaume? Jibu ni kwamba, mwanamke hufana starehe kwa kushirikiana na mwanaume na wanaume ndio ambao huwataka wanawake kushiriki nao katika starehe.

Hata hivyyo, anayeonekana kuwa ni mpenda starehe ni mwanaume na si mwanamke. Hii ni elementi ya mfumo dume ambapo mambo mabaya yote husukuiwa mwanamke hata kama mambo hayo yanamhusu mwanaue pia. Katika riwaya ya *Utengano* tunaona mwanamke akisawiriwa kama kiumbe mpenda stsrehe kama ifuatavyo:

> *Nafasi Mussa alipewa. Akathibitisha udhati wake kwa majani mawili ya shilingi mia mia yaliyomtoka usiku ule. Wakanywa na kuburudika kwa vileo na mazungumzo matamu matamu pale kikaoni pao. Saa nane za usiku ndipo walipotawanyika. Mussa alipewa ahadi kuonana na kazija siku iliyofuata* (uk. 04).

Maneno haya ni uthibitisho tosha kuwa wote mwanaume na mwanamke wanashiriki katika starehe. Dondoo halionyeshi kwamba ni mwanamke pekee ndiye ambaye anashiriki katika starehe. Tena, dondoo linaonyesha kuwa mwanaume ndiye ambaye ametoa fedha kwa ajili ya kugharamia starehe baina yake na mwanaume. Katika uhalisia, daima mwanamke ndiye ambaye hutajwa kuwa ni mpenda starehe na ndiye hushawishi wanaume washiriki katika katika starehe hali ya kuwa si kweli. Huu ni mfano mzuri wa namna mfumo dume unavyofanya kazi katika jamii hususani katika kumkandamiza mwanamke. Wanaufeministi wanalifahamu suala hili vizuri na ndipo pale wanapowataka wanawake kujitambua na kutokukubali kudanganywa ovyo na baadhi ya wanaume na kufanya nao starehe za kiholela (Moore, 1988). Hili linapotokea ni mwanamke ndiye anayehesabiwa kuwa ni muovu hali ya kuwa uovu huo kaufanya kwa kushirikiana na mwanaume.

Pia, mwanamke anasawiriwa kama ni kiumbe ambaye anapenda sana starehe ya kunywa pombe. Hii inaonekana katika dondoo hapo juu lakini tukitazama vizuri tunaona kuwa ni mwanaume ndiye aliyetoa fedha ya kununulia pombe. Hata katika dondoo lifuatalo pia kunajitokeza hali hii:

> *Mussa alipigwa na bumbuwazi. Kila siku anapokuja kwa Kazija huwapo asusa za ulevi, lakini mambo yamezidi. "Mbona gilasi moja tu?" Aliuliza bumbuazi lilipomtoka* (uk. 06).

Dondoo hili linaonyesha kuwa si jambo la ajabu kukuta vileo vya aina mbalimbali katika nyumba ya Kazija. Hii ina maana kwamba, Kazija alikuwa ni mtu wa starehe

na alipenda vileo. Hata hivyo, tunaona kwamba, vileo ambavyo vilikuwa katika meza yake havikuwa kwa ajili yake peke yake bali kwa watu wengi ambao ni wanaume na mmoja wao ni Mussa. Katika hali kama hii lakini bado mwanamke ndiye anayelaumiwa kuwa ni mpenda starehe (Momanyi, 2000). Pia, vileo ambavyo vinapatika katika nyumba ya Kazija vimenunuliwa kwa fedha za Mussa na baba yake ambaye ni Mzee Makusudi-wote hawa ni wanaume. Sasa inakujaje mwanamke ndiye aonekane kuwa yeye ni kiumbe mpenda starehe? Bila shaka ni mfumo dume ambao umeota mizizi katika jamii ndio humuona mwanamke kama kiumbe muovu na mpenda starehe. Hii hawezi kukubalika hata mara moja kwa kuwa inashusha hadhi na thamani ya mwanamke katika jamii (Sengo, 2009).

Katika jamii ya leo kuna mabadiliko kidogo ambapo wanawake wamejitambua na kuanza kujishughulisha kwa shughuli mbalimbali za kuwaingizi kipato na hivyo ile dhana kuwa mwanamke ni kiumbe wa kununuliwa kila kitu inapungua. Mwanamke anayetaka kupata starehe kama ya ulevi hununua vileo kwa pesa zake mwenyewe na wakati mwingine huingia ndani kwake akaendelea na starehe yake. Ile dhana ya kwamba ni lazima akae baa akisubiri apate mwanaume wa kumnunulia pombe inaanza kutoweka taratibu. Hii inawajengea wanawake heshima na kutodhaurauliwa kwa kejeli na kashifa kuwa wao ni wapenda starehe.

4.2.3 Mwanamke ni Malaya

Dhana ya kwamba mwanamke ni kiumbe malaya si ngeni katika ulimwengu wa fasihi na hata katika masikio ya watu katika jamii (Ramadhan, 2013). Malaya ni mwanamke ambaye anakuwa na mahusiano na wanaume nje ya ndoa kwa malengo

mbalimbali ikiwemo kupata fedha. Wapo wanawake ambao wameolewa kwa kufuata taratibu zote za kijamii, kidini na kisheria lakini hutoka nje ya ndoa zao na kuwa na mahusiano na wanaume wengine. Pia, wapo wanawake ambao hawajaolewa na hivyo kuamua kufanya biashara ya ngono kwa kuiuza miili yao kwa wanaume ili waweze kupata fedha za kujikimu. Maelezo haya yanabainisha umalaya unaofanywa na mwanamke si wake peke yake bali wapo wanaume ndani yake. Mwanamke hawezi kuwa malaya kama hakuna mwanaume anayehitaji malaya. Hii ni sahihi kusema kwamba, wote mwanamke na mwanaume ni malaya (Sengo, 2009). Mwandishi ameisawiri hali hii na hapa anasema:

> *Wakapita ndani na bwana Makusuudi akajipweteka kwenye sofa. Alikwenda kitandani akachukua moja katika kanga mbili alizokwisha zifukiza. Kisha akafululiza mpaka pale penye sofa ambapo bwana Makusuudi aliyekwisha vua kofia alikuwa kaka. Kazija alijitupa kwenye sofa ubavuni pa Bwana Makusuudi, na kwa sauti nyororo alianza: "Leo nitakuvua koti mimi."*
>
> *"Ah, hapa… hapana ne… neno, "Bwana Makusuudi alibabaika.*
>
> *"Hebu uko, "sauti ya kazija ilizidi kulegea.*
> *Kazija aliingia kazini huku Bwana Makusuudi akikenuakenua na kutabasamu. Aliona leo mapya. Hakuwa na jingine ila kutii amri* (uk. 11).

Maneno ya dondoo hili yanathibitisha kuwa Kazija alikuwa ni mwanamke mwenye uhusiano wa kimapenzi na Bwana Makusuudi ambaye ni mume wa mtu. Hii ni ishara kuwa bibi huyu alikuwa ni malaya. Maneno kuwa leo ni mimi nitakuvua koti," yanatufanya tuamini kuwa Kazija amekuwa na mahusiano ya muda mrefu na Bwana Makusuudi. Hata hivyo, maneno ya dondoo yanataja bayana kuwa waliokuwa katika huo umalaya si Kazija peke yake bali na Bwana Makusuudi. Kwa hiyo ni sawa na kusema kwamba Bwana Makusuudi licha ya kuoa na kuwa na watoto naye alikuwa ni malaya aliyekuwa na uhusino na wanawake wengine tofauti na mke wake.

Katika uhalisia hivi ndivyo mambo yanavyofanyika ambapo wapo wanaume wanaotoka nje ya ndoa zao na kuwa na wanawake wengine wanaojulikana kwa jina maarufu la nyumba ndogo. Hupeleka mahitaji yote muhimu katika nyumba ndogo hiyo na wakati mwingine mke wa ndoa hukosa mahitaji muhimu kwa sababu ya mke mdogo anakuwa na mahitaji makubwa zaidi. Huu bila shaka ni umalaya wa juu unaofanywa na wanaume lakini daima mwanamke ndiye ambaye analaumiwa (Lyatuu, 2011). Lazima ifike mahali jamii itambuwe kwamba suala la umalaya katika jamii si la mwanamke peke peke yake bali ni la watu wote wakiwemo wanaume na wanawake. Hii itasaidia hata katika harakati za kukomesha umalaya katika jamii. Leo hii tunaona namna serikali inavyojitahidi kupambana na wanawake malaya wanaojiuza katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, Iringa, Moshi na kwingineko lakini hawafanikiwi kwa sababu inamuona mwanamke kuwa ndiye malaya na kusahau hata wanaume ni malaya pia. Ilifaa jitihada hizo ziende mbali zaidi na kumhusisha mwanaume ambaye ndiye mdau mkuu katika masuala ya umalaya. Wanaufeministi wanaamini kwamba, jitihada za kukomesha vitendo vya umalaya zitafanikiwa pale tu wanaume na wanawake watakapojitambua na kuamua kubadili tabia kwa kujua kwamba siku hizi kuna ugonjwa hatari wa UKIMWI unaotokana na ngono za wapenzi zaidi ya mmoja. Jitihada zifanywe kwa kuwalenga wanaume na wanawake na si kundi moja tu.

4.2.4 Mwanamke ni Kiumbe Muovu

Mwanamke ni kiumbe ambaye anasawiriwa kuwa ni muovu wa aina tofautitofauti ikiwemo kufitisha watu waopendana wakawa maadui wakubwa (Momanyi, 2009). Katika jamii inasaidikika kuwa ni kutokana na uovu wa mwanamke ndio maana leo

hii kuna matatizo mengi kama maradhi, njaa, ujinga, chuki, uchoyo, fitina na kadhalika. Mwanamke ndiye ambaye alimshawishi Adamu kula tunda ambalo walikatazwa na Mungu wasilile. Hii ndiyo inayowafanya wanajamii kuwa na imani kwamba mwanamke ni mama wa maovu katika jamii. Mwandishi anaonekana kuungana mkono na mtazamo wa wanajamii ambapo naye amemsawiri mwanamke kama kiumbe ambaye ni muovu na anaweza kuleta maafa katika jamii. Katika dondoo lifuatalo anasema:

> *... Yakanijia mawazo. Nikaona fursa ndio hii. Nikamwita chemba huyu mtoto wake. Nikamtia maneno. Nikamjaza pampu. Akajaa tele. Twende kwa mkunga, miye peke yangu naogopa. Buibui liko wapi, tukatoka, hata mama mtu hana habari. Kiba kibandika, kiba kibandua… Madhumuni hasa ni mkumtia mtoto mjini. Naye keshaingia. Ndani hatoki, hatoki, hajatolewa tu! Tukenda huko nyumbani, tukambawibu mamaake. Akeshazaa tu naye atoke* (uk. 32).

Dondoo hili ni mfano mzuri wa namna mwanamke alivyokuwa kiumbe muovu ambapo tunaona akimdanganya Maimuna ambaye ni mtoto wa Bwana Makusuudi atoke nyumbani kwao bila ruhusa ya wazazi wake. Nia yeyewe ya kumtoa nje ni ili kumtafutia wanaume watakaoanza naye kufanya mapenzi. Huu kwa hakika ni mfano mzuri wa uovu wa mwanamke katika jamii. Si jambo zuri kwa mtoto wa kike kutoka nyumbani kwao bila ruhusa ya wazazi wake kwani hawatajua ni wapi anapokwenda na anakwenda kufanya nini kwa muda gani. Binti Kocho ndiye ambaye alikuwa na lengo hilo ovu la kumpoteza Maimuna kama kisasi kutokana na tabia mbaya ya baba yake ambaye ni Bwana Makusudi kutembea na wanawake wengi na hatimaye kuwatelekeza. Maimuna ni mtoto mdogo ambaye hakuwa na kosa na wala anayoyafanya baba yake yeye hayamuhusu hata kidogo. Lakini anafanyiwa uovu wa hali ya juu ambao baadae ulimfanya kuwa mwanamke asiyeshikika na asiyesikia la muadhini wala mnadi swala.

Katika jamii ya leo wapo wanawake ambao wana sifa kama hii ya kuwapoteza watoto wa wenzao kutokana na wivu au wakati mwingine visasi ambavyo haviwahusu watoto. Hii ni tabia mbaya na haifai kuvumiliwa hata mara moja katika jamii. Bi. Farashuu aliamua kumdanganya Maimuna ambaye ni mtoto wa Bwana Makusuudi na Bi. Tamima aondoke nyumbani kwao aende mtaani. Haya yanabainika zaidi katika dondoo lifuatalo:

> *"sikiliza, mimi nitatoka sasa hivi. Nitatoka, wewe utasubiri kidogo. Ukeshachukua baibui lako utoke; lakini hakikisha kuwa unatoka kwa siri. Usionekane na mtu yeyote. Fuata barabara moja kwa moja, hutokwenda mbali sana, utanikiuta mimi nimepoa nakungojea. Ukitoka ujifunike gubigubi. Usiku wa leo utalala kwangu. Kesho asubuhi nitakwenda kuficha pahala. Babaako hatakuona maisha."*
> *"Haya," alikubali Maimuna. Huo utakuwa mwanzo wa uhuru wake. Mambo si haya!* (uk. 40).

Maneno haya ni uthibitisho tosha kuwa mwanamke huyo aliyefahamika kwa jina la Farashuu ni muovu kwani alifanikisha njama za kutorosha Maimuna nyumbani kwao na kumpeleka mtaani ili awe huru kufanya mambo ambayo ni kinyume na maadili. Kwa mfano, inaelezwa kuwa Biti Kocho na Farashuu walimtorosha Maimuna kwa lengo la kwenda kumtafutia wanaume ambao watafanya naye ngono. Huu ni uovu wa hali ya juu mno kwani kitendo hiki ni kinyume kabisa na maadili ya jamii. Katika jamii ya leo wapo wanawake wenye tabia ovu kama hii ambapo hukusanya wasichana na kuwaweka katika danguro kwa lengo la kuwauza kwa wanaume na kujipatia fedha ambazo huwanufaisha wao wenyewe. Vitendo hivi vya kiovu ni hatari sana kwa maisha ya wasichano hao kwa kuwa ni rahisi kupata maambukizi ya UKIMWI na magonjwa mengine ya zinaa. Wanajamii wanapaswa kutambua kwamba kila mtu ana haki ya kuishi maisha ya kiistarabu na ya utu na kwamba uovu kama huo hauruhusiwi katika jamii (Sengo, 2009).

4.2.5 Mwanamke ni Kiumbe Jasiri

Jasiri ni mtu ambaye anatazamwa na jamii kuwa si muoga wa kufanya mambo ambayo anaamini kuwa ni sahihi kufanywa kwa kuwa hayavunji sheria zilizowekwa. Sifa ya ujasiri imekuwa ikitazamwa kuwa ni ya mwanaume na si mwanamke. Mwanamke hutazamwa kama kiumbe wa nyumbani ambaye hawezi hata kusimama mbele ya mumewe kudai haki yake pale anapoona inapokwa (Koda, 2000). Hili zao la mfumo dume ambao upo katika jamii ambao humchukulia mwanaume kama kiongozi wa kila kitu na hili ndilo ambalo linampa mwanaume uwezo wa kuwa jasiri. Mwanamke atakuwa vipi jasiri wakati hana uwezo wa kutoa maamuzi au kumiliki mali katika jamii? Bila shaka yoyote hili ni suala gumu ndio maana pale mwanamke anapojitokeza kwa sura ya ujasiri kila mtu hushangaa kwa sababu si kawaida (Mlacha, 1996). Katika riwaya ya Utengano kuna mfano dhahiri ambao unaonyesha namna mwanamke alivyo kiumbe jasiri. Mwandishi anasema:

> *Labda Binti Kocho ndiye aliyekuwa mtukutu. Kwa ujasiri wake na usemaji, alimwita Maimuna Chemba kumdodofya. "Mwana, mamaako yuko katika hali mbaya, huenda ikawa hatari, hiyari yako. Mwendekeze babaako. Hivyo mumche kwa jambo hili pia? Sikwambii mengine ambayo yamekupa wewe udode na kukosa mangapi mazuri ya ulimwengu…*
>
> *Sana akija babaako sisi tutakuficheni atajuaje? Na akija kwa meno ya juu, nani kamzalisha Tamima? Mimi nitapiga kifua na kuikabili hiyo nakama atakayoiteremsha, si basi?"* (uk. 21-22).

Dondoo hili linathibitisha namna Binti Kocho alivyokuwa na ujasiri wa hali ya juu katika nyumba ya bosi wake huku yeye akiwa ni mtumishi tu wanadani. Dondoo hili linaeleza kuwa Bi Tamima ambaye ni mke wa Bwana Makusuudi alikuwa mjamzito ambaye alifikia hatua ya kujifungua. Hata hivyo, wakati huo ulipofika mumewe hakuwepo nyumbani na ilikuwa ni amri kwamba haruhusiwi yeye na mtoto wake

aitwaye Maimuna kutoka nyumbani bila idhini ya Bwana Makusuudi. Bi Tamima alikataa katakata kwenda hospitali au kuleta mkunga pale nyumbani bila idhini ya mumewe wakati hali yake ikiwa mbaya na muda wowote angeweza kupoteza uhai wa mtoto na mama yake. Hii ilikuwa ni ajabu kweli kwani mtu angeweza kupoteza maisha bila sababu za msingi eti kwa sababu mume hajamruhusu kutoka nyumbani bila ruhusa yake na wakati huo mume huyo hayupo nyumbani. Itakumbukwa kuwa wakatika riwaya hii inaandikwa hakukuwa na mawasiliano ya simu ya mkononi na hivyo ilikuwa ni kazi ngumu kwa watu kuwasiliana kwa haraka kama ilivyo hivi sasa (Mbonde, 2004).

Dondoo linaonyesha kuwa Binti Kocho ambaye alikuwa ni mtumishi wa ndani katika nyumba ya Bwana Makusudi hakukubaliana na hali hiyo na kufanikisha kumleta mkunga ambaye alijulikana kwa jina la Farashuu. Mkunga huyo alifanya kazi yake na kumsaidia Bi Tamima kujifungua salama salimini. Huu ni ujasiri wa hali ya juu ambapo mama na mtoto wake walishindwa kutambua kwamba ni muhimu mkunga aitwe ili kuokoa maisha mama na kiumbe kilichopo tumboni kwa kumuogopa baba lakini mtumishi wa kazi za ndani Binti Kocho alifanya maamuzi baada ya mashauriano na Maimuna. Binti Kocho aliyafanya haya akiwa anatambua kwamba Bwana Makusuudi akiyajua atamfukuza kazi lakini hakujali kwani alijua kwamba hawezi kufanya kazi kwa Bwana Makusuudi milele.

Katika maisha halisi ya jamii si jambo la kawaida kuona mwanamke tena mtumishi wa ndani kuwa jasiri kama alivyokuwa Binti Kocho. Kama mke au mama mwenye nyumba anakuwa ni muoga na anakosa ujasiri mbele ya mumewe vipi mtumishi wa

ndani anaweza kuwa na ujasiri kiasi hicho? Hii ni ishara njema kwamba fikira za ukombozi wa mwanamke zimeanza kuzaa matunda. Binti Kocho ni kiwakilishi kizuri cha watumishi wa ndani ambao wanaonekana kuwa na msimamo wa kimapinduzi na inapasa kumuunga mkono. Ilizoeleka hapo zamani kwamba mtumishi wa ndani ni kijakazi ambaye anaweza kuteswa kwa kazi nyingi bila huruma na kupata malipo kiduchu. Hili halikubaliki katika ulimwengu wa leo kwani watumishi wa ndani na wanawake kwa jumla wanafahamu haki zao za msingi. Kwa Wanaufeministi hii ni hatua ya juu kabisa ya maendeleo ya mwanamke na inapaswa kuungwa mkono na wanajamii wote wakiwemo wanaume ili kumfanya mtoto wa kike kujiamini na kufanya mambo kwa uhakika bila kuogopa wazazi au mtu mwingine yeyote (Leacock, 1981).

4.2.6 Mwanamke ni Kiumbe Mchapakazi

Mwanamke ni kiumbe ambaye amekuwa akifanya kazi nyingi za ujasiriamali tangu karne na karne lakini huwa hanufaiki na ujasiriamali huo. Ujasiriamali ni msamiati uliopata matumzi hapa Tanzania katika miaka ya 1990 na kuendelea lakini shughuli za ujasiriamali zimekuwepo kwa karne nyingi. Wanawake ndio wafanyakazi wakubwa wa kutumainiwa katika shughuli za kilimo, ufugaji, ususi, ufinyanzi, biashara ndogondogo lakini kipato kinachopatikana huwa chini ya milki ya mwanaume. Upo uwezekano mwanaume akawa hajashughulika kabisa katika uzalishaji mali ndani ya familia lakini yeye ndiye mwenye maamuzi ya namna mapato hayo yatakavyotumika. Imetokea mara nyingi mwanamke amekuwa akikosa manufaa na mapato yatokanayo na nguvu na jasho lake yeye mwenyewe. Katika

riwaya ya *Utengano* tunaona mfano mzuri wa namna mwanamke alivyomchapa kazi wa kutumainiwa na familia yake. Mwandishi anasema:

> *Kulikuwa na mbiringishano fulani wa vyombo huko ndani. Wageni wake Farashuu waliokuwa wameukabili mlango, walitambua kuwa waliowandea walikuwa wa macho.*
>
> *"Nadhani wanasukuma mikate, anafanya biashara. Aaa, Bi. Farashuu utamweza wapi wewe, mchumi kwelikweli. Yeye kazi tu, hataki mchezo, Binti Kocho alimwarifu Maimuna. Binti Kocho aligonga mlango. Mara ya kwanza, kimya. Mara ya pili, kimya. Mara ya tatu ndipo sauti ya Farashuu ilipozuka*." (uk. 29).

Katika dondoo hili kunaelezwa kuwa Bi. Farashuu alikuwa ni mwanamke mchapakazi aliyefanya kazi ya kusukuma mikate usiku ili asubuhi awaridhishe wateja wake na yeye kupata mapato mazuri ya kuendeshea maisha yake na familia. Huu ni mfano mzuri unaonyesha kuwa wanawake si watu wa kukaa nyumbani kusubiri mume afanye kazi na kuleta chakula nyumbani huku mke akiwa amejibweteka. Kitendo cha mwanamke huyu kufanya kazi ya kusukuma mikate ni ishara kwamba mwanamke si kiumbe tegemezi kwa mwanaume kwani anaweza kufanya kazi na kujipatia mapato ya kukidhi mahitaji yake ya maisha. Ilikuwa hapo kale ambapo mwanamke alifanya kazi za ndani tu kama kupika chakula, kuosha vyombo, kudeki nyumba, kulea watoto na kufua nguo na mume ndiye aliyetegemewa kuwa ataleta mahitaji yote ya matumizi nyumbani kwake. Huu ni mfano mzuri wa mwanamke ambaye amejitambua na wanawake wote wa leo wanaweza kufanya kazi vizuri sana.

Katika dondoo hapo juu kuna kauli inayosema, "yeye kazi tu," ambayo inafungamana na kauli mbiu ya serikali ya awamu ya tano inayosema, "Hapa kazi

tu.” Hii inatoa taswira kwamba, mwanamke amekuwa kiumbe mchapakazi tangu zamani kwa sababu riwaya ya *Utengano* imeandikwa mwaka 1980 zaidi ya miaka 36 iliyopita lakini inazungumzia masuala ya mwanamke na kazi. Hata hivyo, bado mwanamke anatakiwa kuwezeshwa zaidi ili aweze kufanya kazi zake vizuri kwa sababu mtaji wake ni mdogo ndio maana anafanya biashara ndogondogo. Mwanamke wa leo anatakiwa kupatiwa mtaji wa kutosha ili aweze kuendesha shughuli zake vizuri na zikuwe zaidi. Hivi leo, wanawake ndio wanaolipa ada za watoto wao shuleni na kuwapatia mahitaji yao yote ya msingi. Hivyo, watakapowezeshwa vizuri itakuwa ni manufaa makubwa kwa taifa na kwa vizazi vijavyo.

4.2.7 Mwanamke ni Kiumbe wa Ndani

Dhana ya kwamba mwanamke ni kiumbe wa ndani na hatakiwi kutoka nje hovyohovyo imeshikiliwa sana katika jamii za Waswahili wa mwambao wa pwani ya Afrika ya Mashariki. Mwanamke hutakiwa kukaa nyumbani akifanya shughuli za nyumbani na mume huenda kazini kutafuta riziki (Mwaipopo, 1990). Mwanamke hatakiwi kwenda sokoni au dukani kwani mwanaume ndiye ambaye anatakiwa kufanya mambo yot hayo na kazi ya mwanamke ni kupokea na kupika mume na watoto wale. Ikitokea mwanamke amelazimika kutoka nje ni lazima afuatane na mumewe au maharimu yake kama baba, kaka, ami na mjomba. Lengo la kufanya hivyo ni kwamba, mwanamke ni kiumbe ambaye anaonekana kuwa ni dhaifu na wakati wowote anaweza kudanganywa na wanaume huko barabarani hivyo ni lazima aongozane na mtu mzima. Huu ni mtazamo wa wanaume wengi wa jamii ya Waswahili ambao kimsingi unatokana na wivu tu wa mume dhidi ya mkewe.

Baba wa familia pia humtaka mtoto wake wa kike kutotoka nje na badala yake akae ndani tu mara baada ya kuvunja ungo mpaka pale atakapoolewa kwani kutoka nje ya nyumbani kwao kutatoa fursa kwa vijana kumdanganya na hata kuweza kumpa ujauzito. Bwana Makusuudi alikuwa ni mmoja kati ya wanaume ambaye hakutaka mtoto wake na mkewe watoke nje ya nyumba yao kwani yeye ndiye aliyewapatia kila kitu. Mwandishi katika riwaya ya Utengano anasema:

> *Tena alijililia jitimai ya kutengwa na dunia ukiwa aliozaliwa nao na kutarajia kufa nao. Alilia sana mpaka macho yakamwiva na kufanya viwingu vya kiza. Hakuwa na budi kujikatia kuwa ndio kesha rudi jela. Ulikuwa unyonge usioweza kuvumilika tena. Alikuwa tafrani kwa kila hali. Alilia hata akakaribia kusahau lile lililomkabili mamaake.*
>
> *Binti Kocho ndiye aliyekwenda kumuita Maimuna. Alimkuta machozi kupukupu. Alikuwa katika uzito wa majonzi na kwikwi za kilio.* (uk. 36).

Dondoo hili linaonyesha kuwa Maimuna hakuwawahi kupewa idhini na mumewe kutoka nje ya nyumba yao tangu akiwa mdogo hata sasa amekuwa mtu mzima. Hali hii ilimnyima fursa ya kukutana na watoto wenzake na kucheza kwa pamoja na sasa amekuwa mtu mzima lakini bado anazuiwa kwenda nje. Kitendo hiki kilimfanya kulia kila mara kwa masikitiko makubwa kwamba ni kwa nini yeye hapewi haki ya kwenda nje kucheza na wenzake na kuungana nao urafiki. Kitu kilichomsumbua zaidi ni ile hali hata ya mama yake kutokuwa na ruhusa na kutoka nje ya nyumba yao bali ni Bwana Makusudi tu ndiye aliyetoka nje ya nyumba yao. Alijiunza kwamba mwanamke ni kiumbe wa kukaa ndani na hatakiwi kutoka nje ya nyumba yao kwani kufanya hivyo ni kosa kubwa ambalo halisameheki.

Kimsingi, kumweka mtoto wa kike au mwanamke utawani si kitu kizuri kwani kila

binadamu nana haki ya kuishi maisha anayopenda ili mradi tu havunji sheria za nchi katika maisha aliyochagua kuyaishi (Mlacha, 1996). Kitendo cha watoto wa kike kuwekwa utawani kimesababisha watoto wengi wa kike kukosa elimu kwa sababu hawkuruhusiwa kwenda shuleni. Ni watoto wa kiume tu ndio ambao walikuwa wanaruhusiwa kwenda shule kwa sababu wao hawana kizuizi cha kukaa ndani kama watawa. Kumuweka mtoto wa kike utawani yaani kumfanya yeye kuwa ni kiumbe wa ndani kunamwadhiri mtoto au mwanamke kisaikolojia na anaweza kufanya mambo ambayo ni hatari kwa maisha yake. Kwa mfano, mtoto ambaye anakatazwa kutoka nyumbani kwao anaweza akachukua uamuzi wa kutoroka na asijulikane alipo na huko akafanya mambo mabaya. Katika jamii ya leo kuna mifano halisi ya watoto wa kike ambao hutoroka nyumbani kwao na kukimbila mijini ili wapate uhuru ambao wameukosa wakiwa katika himaya ya wazazi wao. Wanapofika mjini hukutana na hali mbaya ya maisha na kujiingiza katika vitendo vya kujiuza. Wazazi makini wanapaswa kutambua kuwa uhuru kwa kiumbe binadamu ni kitu cha asili na hata kikizuiwa kwa namna gani lazima tu atakitafuta ili akipate. Ni vizuri wazazi wakawa wanawapa watoto wao uhuru lakini wenye mipaka ili wasione kama wamekuwa wafungwa ndani ya nyumba zao.

4.2.8 Mwanamke ni kiumbe Mtiifu

Mwanamke ni kiumbe ambaye anatazamiwa kuwa mtiifu wa hali ya juu kwa wazazi, walimu na kwa mume mara baada ya kuolewa. Mtazamo huu unatokana na maumbile ya mwanamke kuwa ni kiumbe mtulivu mwenye huruma na asiyekuwa na makuu. Pia, mfumo dume katika jamii umemfanya mwanamke kuwa ni mtu wa daraja la pili ikilinganishwa na mwanaume ambaye ni daraja la kwanza. Hali hii

imemfanya mwanamke kuwa ni mtu wa kutii kutoka kwa mwanaume kila kitu ambacho mwanaume atasema. Hata hivyo, si wanawake wote ambao wamekuwa na sifa hii ya kutii kila kitu laikini bado wanawake wengi ni watiifu. Mfano mzuri wa mwanamke mtiifu ni Bi Tamima ambaye alikuwa ni mke wa Bwana Makusuudi. Mwandishi anasema:

> *"Mama usifanye mchezo 'vyo. Ikiwa kuogopa kuvunja miiko ya nyumba hii, tusiogope. Naivunjwe leo hiyo miiko. Hujui utazaa vipi, mama. Tutangojea idhini ya mtu asiyekuwepo, wala tusiyemtarajia kurudi saa hizi? Hatorudi hapa mpaka wiki iishe. Basi yeye baba hatofahamu kuwa ilibidi tuchukue hospitali au tumwite mkunga hapa?"*
>
> *Mtoto alishauri vyema bali mamamtu alichelea. Aliogopa hasira za mumewe. Vitimbi vyake Bwana Makusuudi havikuwa vidogo siku hizi.* (uk. 36).

Dondoo hili linazungumzia namna Maimuna alivyokuwa akimsahuri mama yake kuchukua uamuzi wa kwenda hospitali au kumuita mkunga wa kumzalisha bila ya kusubiri mpaka Bwana Makusuudi arudi. Maimuna alitambua kuwa hali ya mama yake haikuwa nzuri na hivyo uamuzi wa haraka ulitakiwa ili kuweza kunusuru maisha yake na ya mtoto pia. Kwa kulitambua hili ndio maana alimshauri mama yake akubali kwenda hospitali au kumuita mkunga bila idhini ya mume wake. Bi. Tamima hakukubali mawazo na maoni ya mtoto wake kwani alijua kufanya hivyo ni kuvunja amri ya mumewe kitu ambacho hakuwa tayari kukifanya. Maneno ya Bi Tamima kwamba, "Mm-u, mm-u … babaako hataki tutoke nje ila kwa ruhusa yake, Bi Tamima alimeza maumivu," yanabainisha utiifu wake kwa mumewe. Na kweli Bi Tamima hakukubali maoni hayo ndipo Binti Kocho alimshauri Maimuna kwamba wao wamuite mkunga bila idhini ya mama yake na kweli wakafanya hivyo. Lakini Bi Tamima hakuwa tayari kukubaliana na maoni ambayo aliyaona kuwa yanakiuka

amri na maelekezo ya mumewe hata kama kulikuwa na athari kwake kutokana na kutochukua uamuzi wa haraka wa kwenda kinyumke na maagizo ya mumewe.

Katika ulimwengu wa leo wapo baadhi ya wanawake wenye utiifu kama wa Bi Tamima lakini asilimia kubwa ya wanawake hawana utiifu kama huu. Hii ni kwa sababu katika maisha ya siku hizi kumekuwepo na kampeni nyingi za kuwahamasisha wanawake kutambua haki zao na kuzidai pale inapobidi bila kujali wala kumuogopa mtu yeyote. Suala la mwanamke kujifungua salama ni haki yake ya msingi na haitakiwi kusubiri mpaka mtu fulani atoe ruhusa. Kitendo cha kusubiri mpaka kupatiwa ruhusa ya kwenda hospitali kinaweza kusababisha mama na mtoto kupoteza maisha yao. Hivyo, kisa hiki cha Bi Tamima ni funzo kwa wanawake wote kuwa mwaamke kujifungua salama ni haki yake na haitakiwi kusubiri baraka kutoka kwa mtu yeyote yule awaye.

4.2.9 Mwanamke ni Kiumbe wa Kuteswa

Katika jamii nyingi za Kiafrika mwanamke amekuwa ni kiumbe wa kuteswa kwa namna mbalimbali kama vile kisaikolojia na kimaumbile. Imetokea katika jamii mwanamke apingwa na mumewe kutokana na kufanya kosa fulani kiasi hata cha kumsababishia ulemavu au kifo. Tafiti zinaripoti kuwa baadhi ya wanawake duniani hupoteza maisha yao kutokana na vipigo kutoka kwa wanaume au waume zao. Kitendo hiki si kizuri hata mara moja kwani kinasababisha kumnyima mwanamke haki yake ya msingi ya kuishi kinyume na katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mikataba pamoja na itifaki za kimataifa kuhusu haki za binadamu. Kitendo cha mwanamke kupigwa na mumewe kimejitokeza katika riwaya ya

Utengano ambapo Bwana Makusuudi ameonekana kumpiga mkewe tena katika hali ya uzazi. Mwandishi anasema:

> *Maimuna yu wapi naseeeemaaaa. Ilikuwaje? Alaa, ndio mambo yako haya? Nikiondoka mimi, wewe hutawala enn? Unamtorosha mwanangu na wewe mwenyewe unajiuza siyo? Yuko wapi Maimuna? Makusuudi ilimtoka bakora ambayo ilianguka juu ya kichwa cha Tamima. Tamima alipiga usiyahi mkubwa akaanguka chini. Muda ulipita. Makusudi alihema kwa ghadhabu na Tamima aligaragara. Baadaye Tamima alipopata upumzi, alitupa mkono pale alipopigwa bakora. Damu ilikuwa ikimchururika.* (uk. 47).

Dondoo linaeleza kuwa Bwana Makusuudi alimpiga Tamima ambaye alikuwa ni mkewe bakora ya kichwani na kusababisha damu kuchuruzika. Katika hali ya kawaida huu ni unyanyasaji na utesaji wa mwanamke. Kichwa ni sehemu hatari katika mwili wa binadamu kwa sababu ndipo mahali penye ubongo na ubongo ndio unaoufanya mwili ufanye na usifanye nini. Halikuwa kosa la Tamima kuondoka kwa Maimuna bali ni kosa la Bwana Makusuudi kumzuia binti yake asiwe huru kutoka nje kukutana hata na rafiki zake. Upweke aliokuwa nao Maimuna ndio ulimfanya kupata fikira za kutoroka nyumbani ili apate uhuru wa kuwa na maisha yake. Kibao kimemgeukia Tamima na sasa yeye ndiye ambaye anaonekana kuwa mkosaji wa kitendo cha Maimuna kutoka nyumbani. Kipigo alichokipata kutoka kwa mumewe kinatosha kuwa na athari kubwa kwake kisaikolojia na kimaumbile.

Katika jamii ya leo wapo wanaume ambao huwapiga wake zao kutokana na sababu mbalimbali na baadhi ya wanawake wameshapoteza maisha. Hii inatokana na mfumo dume uliopo katika jamii ambao unamtazama mwanamke kama kiumbe ambaye hajakamilika na ni mkosaji tu. Baadala ya kutumia njia nzuri za kumuonya, baadhi ya waume huamua kuwapiga wake zao ikiwa kama ndio kumfundisha adabu ili

asirudie tena. Imetokea katika baadhi ya jamii za Kitanzania kwamba mwanamke asipopigwa na mumewe basi mume huyo anakuwa hampendi mkewe (Shao, 2003). Hali hii inalawalazimisha wanaume wawapige wake zao ili wajuwe kwamba wanapendwa.

Kimsingi, huu si mtazamo sahihi na unapaswa kupigwa vita kwa nguvu zote. Kwa Bi Tamima yeye haikuwa hivyo, aliamini kwamba kumpiga mwanamke ni kinyume na haki ndio maana alikuwa akimuomba mumewe msamaha kwa kitu ambacho hakufanya yeye lakini mumewe aliendelea kumpiga. Mwandishi anasema:

> *"Ni… sameeeeehe Bwana Makusuudi si kosa languuuuuu; Maimu … na kakimbiaaaa… Makusudi alitupa bakora yake na sasa aliupapatua ukanda wake kiunoni. Aliuvuta na kuanza kumcharaza nao mkewe* (uk. 48)."

Bwana Makusuudi kama lilivyo jina lake alitambua kwamba mwenye kosa ni yeye kwani ndiye aliyemnyima mtoto nafasi ya kuwa huru na ndio maana ametoroka nyumbani. Lakini kwa kukosa huruma na mapenzi ya dhati alimwadhibu Tamima bila sababu na huku akitambua kuwa ndio kwanza alikuwa amejifungua. Huu ni unyanyasaji na utesaji wa kijinsia ambao hautakiwi kuvumiliwa katika jamii ya Watanzania na duniani kote. Wanaufeministi wamefanya kazi kubwa ya kuielimisha jamii kuhusu kuacha ukatili wa kijinsia na matunda mazuri tayari yameshaanza kuonekana. Tunaishauri jamii imheshimu na kumjali mwanamke ambaye ndiye mlezi na mama wa watu wote duniani.

4.3 Hitimisho

Katika sura hii tumewasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti wetu tukizingatia malengo mahususi mawili. Malengo hayo yalikuwa ni kuchambua

usawiri wa mwanamke katika riwaya ya Utengano na kisha kuelezea uhalisia wa dhamira hizo kwa jamii ya leo.

SURA YA TANO

5.0 HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Hii ni sura ya mwisho katika tasinifu hii ambayo inatoa hitimisho la utafiti mzima. Pia katika sura hii tumetoa muhtasari kwa kila lengo mahususi la utafiti lengo likiwa ni kumpatia mtafiti baadhi ya mambo muhimu yaliyowasilishwa katika kazi yetu kwa muhtasari.

5.2 Muhtasari

Utafiti huu ulikuwa na malengo mahususi mawili ambapo lengo la kwanza lilichambua usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Utengano* na lengo la pili lilikiwa ni kubainisha uhalisia wa usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Utengano* kwa jamii ya leo. Muhtasari wa utafiti umezingatia malengo mahususi hayo mawili ambayo yameunganishwa pamoja kama ifuatavyo.

5.2.1 Usawiri wa Mwanamke katika Utengano na Uhalisia Wake kwa Jamii

Mwanamke amesawiriwa katika nafasi mbalimbali ndani ya riwaya ya *Utengano* ambapo kwa kiasi kikubwa imeonekana kuwa mwanamke ni kiumbe ambaye anafanya jitihada kubwa ya kujikomboa kutoka katika mfumo dume. Matokeo ya utafiti yanabainisha kuwa mwanamke ni kiumbe tegemezi kwa mwanaume, mwanaume ni kiumbe mpenda starehe, mwanamke ni malaya, mwanamke ni kiumbe muovu, mwanamke ni kiumbe jasiri na mwanamke ni kiumbe mchapakazi. Pia, matokeo ya utafiti yanabainisha kuwa mwanamke ni kiumbe wa ndani, mwanamke ni kiumbe mtiifu na mwanamke ni kiumbe wa kuteswa. Kwa hakika, riwaya ya

Utengano imemsawiri mwanamke katika hali ambazo tunaziona zikitokea hata katika maisha halisia ya jamii ya leo. Zipo baadhi ya jamii ambazo zinamtazama mwanamke kama kiumbe asiyeweza kufanya kazi na kujitegemea. Hawa ni baadhi ya watu ambao huwafanya wake zao kuwa ni watu wa ndani wasioruhusiwa kutoka nje kwenda kufanya kazi. Sababu kubwa ya kufanya haya ni wivu tu ambao huwakumba baadhi ya wanaume wakidhani kuwa kuwaruhusu wake zao kwenda kufanya kazi kutasababisha wapate wanaume wengine. Kiuhalisia tumeona kuwa jambo hili kwa sasa limepungua mno na hata kama wapo ni wanaume wachache wenye mtazamo kama huo. Wanaume wengi wanawaruhusu wake zao kufanya kazi ili kupata kipato kwa ajili ya kutimiza mahitaji ya familia.

Matokeo ya utafiti yanabainisha kuwa mwanamke anasawiriwa kama kiumbe ambaye anapenda sana starehe. Mwanamke anasawiriwa kuwa ni mtu ambaye anapenda starehe za kunywa pombe na kushiriki ngono na wanaume na kwamba analaumiwa kwa hilo.

Katika utafiti huu imebainika kuwa mwanamke huwa hawafanyi starehe mwenyewe bila ya mwanaume na wanaume huwa ndio huwa wanawataka wanawake kufanya nao starehe. Pamoja na ukweli huu ni mwanamke peke yake ndiye ambaye anaonekana ni mpenda starehe. Hii bila shaka ni uonevu kwa jinsia ya kike na inatokana na kuwepo kwa mfumo dume katika jamii. Wanaume hutaka kuonekana kuwa wao ni watu safi na wakamilifu na wanawake ndio wakosefu. Hii si sahihi hata kidogo bali katika uhalisia tunatambua kuwa starehe ni kitu ambacho kinapendwa na wanaume na wanawake pia.

Matokeo ya utafiti yanaendelea kubainisha kuwa mwanamke anasawiriwa kama kiumbe ambaye ni muovu. Hii inajitokeza pale ambapo mhusika anayejulikana kwa jina la Farashuu akishirikiana na Binti Kocho wanapomtorosha Maimuna kutoka nyumbani kwao na kumpeleka mtaani. Kitendo hiki hakikuwa kizuri hata kidogo na hakipaswi kufanywa na mtu yeyote yule awaye katika jamii. Katika jamii ya leo pia wapo baadhi ya wanawake ambao kwa makusudi hutumia njia za hila kuwapotosha watoto wa wenzao katika jamii. Mtoto akishazaliwa huwa ni rasilimali muhimu ya taifa na hivyo anapaswa kuongozwa katika misingi mizuri ya maadili yanayokubalika katika jamii.

Pia, Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa mwanamke anasawiriwa kama kiumbe ambaye ni jasiri asiyeogopa kitu katika kutetea ukweli na haki yake. Binti Kocho amethibitisha kuwa mwanamke ni kiumbe jasiri pale ambapo alisimama kidete kumtetea Bi Tamima kuwa hakuhusika katika kumtorosha Maimuna dhidi ya Bwana Makusuudi. Binti Kocho alikubali kupoteza kazi yake lakini atetee haki na ukweli na alifanya hivyo. Katika jamii ya leo tumeona namna wanawake walivyokuwa na ujasiri wa kutetea na kudai haki zao bila uoga wala aibu ya aina yoyote. Mfano wa Binti Kocho unapaswa kuigwa na wanajamii ili kuhakikisha usawa wa kijinsia unapatikana katika jamii.

5.3 Hitimisho

Kwa jumla, riwaya ya *Utengano* ni riwaya ambayo bado inaeleza mambo yenye uhalisia katika jamii ya leo na ni vema ikaendelea kusomwa katika ngazi mbalimbali za elimu hapa nchini. Riwaya hii imeandikwa mwaka 1980 ambapo mpaka sasa ni

miaka 36 lakini mambo inayoeleza kumhusu mwanamke yana uhalisia. Imebainika kuwa ili kupata ukombozi wa kijinsia ni lazima kuwe na ushirikiano baina ya wanaume na wanawake. Hili litafanikiwa vizuri pale wanaume watakapobaini kuwa mwanamke ni kiumbe kama walivyo wao na hivyo ni wajibu kusaidiana ili kufanikisha azma ya kuleta usawa wa kijinsia. Mwanaume na mwanamke ni watu wanaotegemeana na kila anachokifanya mmoja wao kina athari kwa mwingine. Mfano wa Bwana Makusuudi kumpiga mkewe bila kufahamu ukweli wa mambo ulivyo ni kitendo kisichokubalika wala kuvumilika. Ni vema wanajamii wakaelewa umuhimu wa kila mwanajamii kusikilizwa kabla ya kuchukua uamuzi wa kufanya jambo fulani. Hii inatufanya tuhitimishe kuwa elimu kwa jamii kuhusu usawa wa kijinsia ni kitu muhimu ambacho kinatakiwa kuwa endelevu na kisipuuziwe. Hii itaifanya jamii kuishi katika maisha ya usawa wa kijinsia.

5.4 Mapendekezo

Utafiti wetu hakuchunguza mbinu za kisanaa na hivyo tunapendekeza mbinu za kisanaa zitafitiwe na watafiti wajao kwani riwaya ya Utengano ina matumizi ya mbinu nyingi za kisanaa.

Utafiti zaidi unaweza ukafanywa juu ya namna jina la kitabu cha *Utengano* linavyolandana na yale mambo ambayo yanaelezwa ndani ya riwaya hiyo.

MAREJELEO

Babbie, E. (1999). *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth.

Bouchier, D. (1983). *The Feminist Challenge*. London: Macmillan Press.

Chachage, S. C. (1991). *Almasi za Bandia*, Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Chachage, S. C. (2002). *Makuadi wa Soko Huria*, Dar es Salaam: E&D Company.

Cohen, A. (2000), *Research Methods in Education*. London: Routledge Falmer.

Eisenstein, Z. (1979). "Capitalist Patriarchy and Case for Socialist Feminism in New York," Monthly Review.

Hussein, E. (1970). *Wakati Ukuta*. Nairobi: EAPH.

Hussein, E. (1971). *Mashetani*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Hussein, E. (1976). *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi*. Nairobi: Oxford University Press.

Hussein, E. (1980). *Arusi*. Nairobi: Oxford University Press.

Hussein, E. (1988). *Kwenye Ukingo wa Thim*. Nairobi: Oxford University Press.

Kamba, T. P. (2012), "Usawiri wa Muhusika Mwanamke katika Tamthilia ya *Kilio Chetu* na *Nguzo Mama*". Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Khatib, M. S. (1986), "Uchambuzi wa Riwaya ya Kuli" Katika *Mulika* Namba, 9, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, TUKI.

Kiango, S. D. (1992), Taswira ya Mwanamke katika Tamthilia za Kenya. Katika *Baragumu* juzuu ya 1 na 2 Kenya: Jarida la Kiswahili Chuo Kikuu cha Masemo.

Koda, B. (2000) "The Gender Dimension of Land Rights in Tanzania: Case Study of

Msindo Village, Same District", Unpublished *Ph.D Thesis*.

Kothari, C. R. (2008). *Research Methodology; Methods and Techniques*, New Delhi: New Age International (P) Limited

Lyatuu, J. (2011). Usawiri wa wanawake katika fasihi ya Kiswahili: Ulinganifu wa waandishi wa kike na kiume uchaguzi katika riwaya Teule. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Macknnon, C. A. (1991). *Toward A Feminist Theory of State*. London: Havard University Pess.

Matteru, M. O. B. (1982). "The Image of The Women in Tanzania Oral Literature." "A survey" katika *Kiswahili*, Jarida la TUKI Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Vol 41(2).

Mbonde, J. P. (2004). "Chachage Seithy L. Chachage: *Makuadi wa Soko Huria* (2002), Uchambuzi na Uhakiki," katika Swahili Forum 11, 214-226.

Mlacha, S. A. K. (1996). "Women Images in Kiswahili Poetry & Taarab Songs*",* in D. Mbilinyi & C Omary (Eds): *Gender Relation & Woman Media*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mnenuka, A. (2011). "Taswira ya Mwanamke katika Muziki wa Bongo Fleva: Mifano kutoka katika Nyimbo Teule." Katika *Mulika* Na 29 &30 Toleo Maalum la Kizazi Ki

Mohamed, S. M. (1978). *Nyota ya Rehema*: Nairobi: Oxford University Press.

Mohamed, S.A. (1980). *Utengano*, Nairobi: Longman.

Momanyi, C. (2000) "Usawiri wa Wahusika wa Kike katika Fasihi ya Kiswahili baada ya 2000: Kuyumbisha Uhalisia", katika I. S. Mdee & H. J Mwansoko: *Makongamano ya Kimataifa ya Kiswahili*, Dar es Salaam: TUKI

Momanyi, C. (2009). “Nafasi ya Mwanamke katika Ushairi wa Shaaban Robert” katika *Kiswahili* 64, 53-63. Dar es Salaam: TUKI.

Moore, H. (1988). *Feminism and Anthropology*. Mimepolis: University Press of Minnesota.

Muhando, P. M. (1982). *Nguzo Mama*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mule, K. (2004). “Theatre and Development: Mordern East African Women Playwright and Critique of Development”. Katika Jarida la Kiswahili, 67, 49-78, Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M. M. (1982). “Protest and Resistance in Swahili Poetry 1600-1885”, katika *Kiswahili* 45(1), 25-54.

Mulokozi, M. M. (2012). “Makuadi wa Soko Huria (Chachage S. Chachage) katika Muktadha wa Riwaya ya Kihistoria katika Fasihi ya Kiswahili,” Katika *Mulika* 31, 51-66, Dar es Salaam: TUKI.

Mwaipopo, R. N. G. (1990). “The Impact of Commodity Relations on the Role and Status of Women in Peasant Households: A Case Study of Rungwe District”, M.A Thesis, University of Dar es Salaam, Tanzania.

Ngaiza, M. K. (2002). “Gender Dynamics in Poverty Alleviation in Tanzania: Ngara District Case Study.” Unpublished, *Ph.D. Thesis*, University of Dar es Salaam, Tanzania.

Ngaiza, M. K. (2003). “Gender and Political Empowerment in the Third Millennium: A Conceptual Frame Work.” In: *Tanzania Journal of Development Studies*, 4(1), 167-212.

Ngaiza, M. K. (2004). “Harmonization and Mainstreaming Gender in Local Government or Transforming Patriarchy: The Case of Two Wards in Bukoba District Council, Tanzania.” In: *Tanzania Journal of Development Studies*, 5(3), 25-38.

Njogu, K. & Rocha, C. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi, Jomo Kenyatta Foundation.

Ntaragwi, M. (2004). Uhakiki wa Fasihi. Rock Island: Augustana College

Omari, S. (2008), Fasihi Simulizi na Jinsia. Katika *Kiswahili* Juzuu ya 71(71), Dar es Salaam: TUKI.

Phillip, L. (2009). A Critical Language Study of Mipasho Taarab and Bongo Fleva. Tasnifu ya M.A (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Tanzania.

Ramadhani, S. K. (2013), “Usawiri wa Mwanamke Katika Taarab ya Mipasho: Mfano Kutoka Nyimbo za Mzee Yussuf Mzee”. Tasinifu ya M.A. Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Tanzania.

Robson, C. (2007). *How to do a Reserch Project*: A Guide for Undergraduate Students, Carton Victoria: Blackwell Publishing.

Sengo, T. S. Y. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi*, Dar es Salaam: AERA.

Shao, I. F. (2003). “Beyond Rhetoric: The Role and Experience of the University of Dar es Salaam Advancing the Involvement of Men in Gender and Development Practice,” In: *Tanzania Journal of Development Studies*, 4(1), 117-125.

Shao, I. F. (2004). *Context for Gender Mainstreaming Internationally, Regionally and Nationally,* Paper Presented at a Gender Sensitization Workshop for UDSM Council Members, Zanzibar.

Shao, I.F. (2010). Gender, Rural Development and Governance: An Overview, In: *Tanzania Journal of Development Studies*, 10(1), 78-87.

Wafula, R. M & Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi.* Nairibi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wegesa, B. N. (1994). "Mwanamke katika Tamthilia za Ebrahimu Hussein". Master of Philosophy, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Yin, R. K. (1994). *Case Study Research: Design ad Methods*, (2nd eds. Thousands Oaks California: SAGE publishers.